# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION
# (CKRC)

## Verbatim Report of

## DISSEMINATION OF REPORT & DRAFT BILL, SABOT CONSTITUENCY, KITALE TOWN – MUSEUM HALL

## ON

## 8TH OCTOBER 2002

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL**
**SABOT CONSTITUENCY – KITALE TOWN – MUSEUM HALL TUESDAY 8/10/2002**

**Present**

Com. Salome Muigai - Commissioner

Com. Dan Tuma - Ass. Programme Officer

**Secretarial in Attendance**

Asenath Kang'a - Verbatim Reporter
Emmanuel Sasia - Coordinator

**Meeting was called to order at 10.15 a.m.**

**Emanuel Sabati:** Karibuni, karibuni sana katika mkutano wetu wa kujadili draft Constitution. Lakini kama kawaida kabla ya kwanza mkutano ningalipenda kumwita Bwana Gerald Njagi ambaye atatuongoza kwa maombi.

**Bwana Gerald Njagi:** Tusimame tuombe. Mungu muumbaji wa wanadamu wote,= ni shukrani nyingi tunakurudishia kwa sababu ya siku hii Bwana umepeana. Tunakushukuru kwa mikutano yote tukijua tumekutana kwa mkutano kama huu Bwana tunakuuliza mwanzo mwema na mwisho wake Bwana tunakushuru. Asante kwa kuleta Commissioner wetu na Bwana tunakuuliza hata wale watu wengine wako njiani wakija uwawezeshe basi tushirikiane pamoja ili tufikie kazi zile Bwana unataka tufanye na Constitution Review ya kazi zetu za Constitution. Mungu wetu tunakuhitaji katika mambo yote, kua Bwana kiongozi. …………… (inaudible) Bwana tushauri ukiona ni vyema Bwana utukemee utukemee, kwa sababu Bwana wewe ni Mungu mwema na unajua mahitaji ya kila mmoja wetu. Nchi yetu ni mikononi mwako na tunajua Bwana utatubariki na kazi yako Bwana itaendelea bila kua na shida yoyote. Na yote tunaomba kwa jina lako aliye Bwana Mkombozi tunaomba. Amen.

**Emanuel Sasia**: Kwa hivyo ningependa kuchukua nafasi hii kuakaribisheni tena na kushukuru kwa kufika kwenu, najua wengi bado wako njiani wanakuja. Lakini kwa sababu mkutano wetu una mambo mengi tungalipenda kuanza mapema ili watu ambao watakua na maswali wapate nafasi nzuri ya kuuliza maswali. Lakini kwanza kabisa Commissioner wetu ningelipenda wale wana kamati wakamati mbali mbali za sehemu mbali mbali za wakilishi bungeni wasimame pote walipo ili wananchi pia wapate nafasi ya kuwaona ili kukiwa na swali labda……… (inaudible) wanaweza kusaidia. Kwa hivyo watu wana kamati tafadhali wale ambao wako hapa ndani wasimame ili kuonekana.

Tukianzia upande wako wa kushoto kabisa Naomi ….. (inaudible ambaye ni mwanakamati katika kikao cha Saboti kisha anafuatwa na Bi Mary Nyambane ambaye pia yuko katika kamati ya Saboti. Kwa mkono wangu wa kulia ni Bi Nancy Yale ambaye pia yuko katika kikao cha kwanza. Bwana Joseph Chebii ni mwakilishi kutoka katika upande wa …… (inaudible) katika …….. (inaudible) wetu alikuwa akimwakilisha Bwana Muheshimiwa Nicholas Gor. Kisha anafuatwa na Bwana Gerald Njagi ambaye ni mwanakamati wa kwanza. Bwana Chemalungu ni mwana kamati kutoka katika eneo la uwakilishi la Kwanza anafuatwa na Bwana Peter Wagara ambaye pia ni wa kutoka upande wa Kwanza kisha ako hapa Cheptas kutoka upande wa Saboti na mwisho kabisa kwa wale wako hapa Rai ni Bi Veronica Kibet ambaye anatoka sehemu ya uwakilishi ya Siritanyi. Mimi ni mshilikishi katika Wilaya naitwa Emanuel Sabati. Karibuni.

Labda kabla tuendele ningalipenda Commissioner kwanza nikuombe utufahamishe kwa wale ulikuja nao na pengine uwape nafasi ya kujitambulisha kwa wananchi ya Sabot karibu.

**Com. Salome Muigai**: Asante sana Coordinator na …… (inaudible) wananchi wa Sabot na Kitale kwa jumla kwa kufika hapa leo, siku ya leo. Mimi jina langu naitwa Salome Wairimu Muigai kwetu ni Eldoret kwa hivyo siko mbali sana na nyumbani najisikia niko nyumbani nikiwa hapa Kitale leo. Tumeandamana na wafanya kazi watatu, mmoja ni Bwana Juma na ni programme officer wetu, pia tuna Bi Kanga Asenath ambaye atakuwa akifanya recording moja kwa moja na pia tuna driver mwenye ametuleta nafikiri bado anashugulika na hali ya gari yuko nje anaitwa Kamau. Oh Kamau yuko pale asante. Hawa ndiyo tumekuja nao kutoka Nairobi.

Leo tutaendelea kujuana zaidi, tukiendelea tafadhali ukipata nafasi ya kuzungumza tueleze jina lako ili tukujue. Sijui mnataka tutumie lugha gani, nilikuwa nimefanya mipango yangu ya kuwasalimia, nilikua nimeanza na *chamge tugul?*

**Audience:** *Chamge tugul.*

**Salome Muigai**: *Mlembe bosi?*

**Audience**: *Mlembe bosi.*

**Salome Muigai**: *Muriega*?

**Augience**: *Turiega.*

**Salome Muigai**: *Muria seyo*?

**Audience**: *Turia seyo*.

**Salome Muigai**: Good. Hamjambo mabibi na mabwana?

**Audience**: Hatujambo.

**Salome Muigai**: Huu ni wakati mzuri wa sisi kuasiliana, na kama nilikuwa nataka kuanza kusema sana ni kua sana sana sisi kwenye tume letu tunatumia lugha ya Kiswahili and Kiingereza, na zaidi ya hayo tunakubalisha mtu azipoweza kuzitumia lugha mbili kutumia lugha yenye ataweza kujielewa nayo. Lakini hilo zaidi nitatumia lugha ya Kingereza zaidi zaidi kwani mambo yenye tunazungumzia leo ya Katiba ni mambo ya kitaalam kabisa, na mambo mengi yalichapishwa kwa lugha ya Kiingereza. Lakini sijui kama kuna mmoja wetu ambao, wengine hawafahamu lugha ya Kingereza hasa kabisa. Kunaye? Kuna mtu ambaye tukizungumza na Kiingereza atakua ameachwa nyuma, tafadhali inua mkono? Huyo mmoja nani mwingine, pia wewe kuna mtu

mwingine? Okay hiyo ni vizuri kuelewa ili nijue wakati wa kufafanunua mambo mengine kwa Kiswahili.

Sasa ningeanza kwa kurudi nyuma kidogo niwaeleze kuwa tume imekua ikifanya kazi kutokea June mwaka uliopita. Kazi ile kubwa ilikuwa kuja kusikiliza maoni yenu na pia kunganisha pamoja yaani to collect and ………(inaudible) your views, na kuyaweka pamoja na kuandika report, na kuwatolea report ya mambo ambayo mulitweleza. Tulifanya hivi na tumetowa report hii, sijui kama watu wengi waliiona kwenye nakala ya magazeti. Mliiona ripoti fupi? The short report? Siyo hii yenyewe nimewapatia leo, hii report ni fupi. Kwa hivyo hii report ndiyo imenieleza mambo gani mliotueleza. Zaidi ya hiyo pia tumekuja na report nyingine leo yenyewe sijui Bwana Sasia tumekuja na report ya kikao hiki cha Sabot, mambo gani tulielezwa Sabot yenyewe? Wakati huu tuna report hiyo ya kikao hiki. Do we have the constituency report?

Kwenye hii file tuna ile mambo yote yenyewe mlietueleza kutokea kikao cha tume cha Sabot, ndiyo mkitaka kuiona mnaweza kuenda kwa afisi ya Bwana Sasia mtaisoma kutoka mwanzo mpaka mwisho. Hii report ya hapa Sabot na report za kutoka vikao vya bunge vingine zaidi ya Sabot kuna vingine ngapi? Mbili Kenya nzima? Au tuna vingine ya Kitale sivyo? Lakini kwenye Kenya zima tuko nayo. Ni ngapi? Mia mbili na tisa sivyo. Kwa hivyo kila tume tumekua na report hii moja tuseme kama sisi tunazo. Tunazo mia mbili na kumi. Kwa hivyo kila kikao ukienda Kisamwani utakuta file kama hii lakini si ya Sabot ni ya wapi? Ni ya Chelangani. Ukienda wapi wengine kikao chenye kinaitwa……………. (inaudible) …..? Mimi ni mwalimu huwezi kukaa hapa bila kufanya kazi ukiwa kwenye darasa langu. Uwaalimu ni interaction kwa hivyo mkuwe tayari mtu asilale nitawauliza maswali.

Basi kikao kingine hiki hapa Kwanza kwa hivyo ukienda Kwanza utapata file imeandikwa nini, report ya Kwanza Constituency. Basi mimi tumeangalia hizo reports zote tukapata kwa ufupi hizo reports zote ndiyo tukapata chaguo wananchi tunaita Peoples Choice ama Chapora Wananchi. Kutokana na hizo support – by the way tunaziita chaguo kwa Kiingereza na pia tunazo kwa Kiswahili. Mimi ninachagua langu kwa Kingereza Peoples Choice na pia na chagua kwa Kiswahili. Hizi zilikua kwenye nakala za gazeti karibu siku mbili tatu zilizopita tulitoa wakati kabla hatujaenda Mombasa. Basi kazi yetu baada ya kuandika hiyo report asubuhi ya leo ilikuwa kuchukua hiyo report na kuiyangalia ile inaweza kutafsiriwa kutoka kwa report hua sheria. Basi kwenyewe tumechukua tumejidiliana, tulichangiliana karibu mwezi mzima. Sisi watu ishirini na tisa ndiyo tulifikiana kile tungetaka, hili ilichukua karibu mwezi mzima. Mwishoni tulikubaliana mambo gani wananchi wanataka kama wanatuambia, ndiyo tuelewane tukatoa the proposals of the Draft Bill. Hii Draft Bill yenyewe sasa tuko nayo kwa nakala ya gazeti ndiyo makubaliano yetu.

Ningetaka kueleza jambo moja juu ya hii Draft Bill. Tulipokua tukizungumzia hii draft bill hakuna hata wakati mmoja tuliokosa kuelewana mpaka tukapiga kura. Tulizungumza pamoja, tukaelewana mambo mengine kwa urahisi, mengine yatachukua muda, na yale hatukuelewana tulisema twendeni tule, ama twende tulale tutaongea hayo kesho asubuhi. Tunaenda tuna kula, tukazungumza, tukalala, na nyakati nyingi pia tukaomba, tukiombea hii Katiba. Mwishoni tuliweza kuelewana bila kupiga kura. Kwa hivyo kila mmoja wetu sisi wanatume tukiwa kule kila mmoja mwenyewe ambaye alikuwa Mombasa ataweza kusema,

kuzungumza ukweli kuwa tulikubaliana na nyinyi kwa hii mswada wa Katiba hii mpya.

Sasa leo tuko hapa kufanya kitu gani? Wacha nisemu kile kitu hatuko hapa kufanya. Hatuko hapa kuelewa hii Katiba mpaka tukiondoka hapa tukipatiwa mtihani kila mtu ataenda Alliance kwa hii Katiba. Mtu mwenyewe atakwenda Alliance atatafuta jambo lingine na siku nyingine. Hii siku moja haitatosha. Hatuko hapa kukubaliana ama kutokubaliana habari ya hii Katiba ama huu mswada. Leo tuko hapa kwa jambo moja, tuko hapa kujaribu kuwa introduced kwa huu mswada. This is a very short introduction of the Proposed Draft Bill. Nitakua na wakati wa kujibu swali moja ama kumi ama ishirini. Lakini hatutakubaliana kuwa kitambo tutoke hapa hakuna mtu mwenye hatakua na swali, ………….. (inaudible) kwani habari ya kutengeneza Katiba sio kikao isio, the activity is a process. Ni kama safari, ninaweza kukaa hapa dakika moja ni kafikilia sasa niko Nairobi, nikitaka kwenda naweza kukaa hapa halafu nitasema nitafika Nairobi? La nifaki na nitahatua kwa nini? Kwa hatua sivyo. Lazima nitoke hapa nifike Moi's Bridge sivyo, halafu nifike Matuda, nifike Eldoret, halafu mwishowe nitasafiri wakati mrefu nitafika Nakuru na hatimaye nitafika Nairobi. Kwa hivyo hii ni safari ya Katiba yetu ni safari, leo ni …. (inaudible) ya kwanza, Waswahili, Wachinese wanasema safari ya kilometer elfu moja huanza na nini? Huanza na hatua moja. Kwa hivyo leo tunaweza kuchukua hatua moja tukiweza tunaweza kuchukua kumi tunaweza kuchukua hatua hamsini lakini bado ni safari. Tukisaelewa hiyo ndio tutaanza safari ya leo.

Jambo la pili, habari ya kufanya introduction ama kujwajulisha kwa Katiba leo ni kazi yangu kama mwanatume. Lakini pia wewe una jukumu, wewe ulioelezwa hata Bibilia Yesu anatwambia wewe uliosikia wewe ufanye nini? Usisikie tu na wewe ushikilie tu mpaka kule unaenda mbinguni ukisha sikia habari njema ama ufanye nini? Ufanye nini?

**Audience**: Ueleze.

**Com. Salome Muigai:** Uweleze wengine. Kwa hivyo wewe ukiondoka hapa na umesha fanyiwa hiyo introduction fupi na wewe una akili yako ama nakala yako ya Katiba uende ueleze wengine. Uende na wewe uanzishe debate pahali pengine. Ukiwa wewe ni mtu mwenye uko afisini uende ukaanze debate na mwenye uko naye afisi pamoja. Ukiwa wewe jamii pia ni wakati wa kuzungumzia habari ya Katiba kwenye nini? Kwenye jamii yako. Ukiwa wewe una kikundi chako kina kutana mara moja kwa mwezi, mara moja kwa wiki, mara kadhaa basi kama ulikuwa unakutakana mwezi ujao tafadhali iteni kikundi cha mkutano wa hadhara wa kikundi chako ili uzungumzie nini? Hii Katiba yetu. Tukiizungumzie hayo tutakuwa na faida mbili. Moja tutaelewa Katiba yetu inasema nini, ya pili tutakubaliana kwa mambo mengine na yenye iko kwa hii Katiba yenye kila pahali yenye tunaenda tuliambiwa jambo ni hilo hilo kama tulipokuja Sabot tukaambiwa hayo, tuliependa Kacheliba tukaambiwa hayo, tuliopoenda Kisauni tukambiwa hayo hayo. Kwa hivyo tuna mambo mengi kwa hii Katiba yenyewe Wakenya wote wanakubaliana.

Jambo kama hili sisi sote tunakubaliana sisi wote ni Wakenya. Tunakubaliana sisi zote ni Wakenya?

**Audience**: Ndiyo.

**Com. Salome Muigai:** Haya sisi zote tunakubaliana tuna makabila tofauti?

**Audience**: Ndiyo.

**Com. Salome Muigai**: Hiyo ni kweli?

**Audience**: Ndiyo.

**Com. Salome Muigai:** Sisi Zote tunakubaliana kuwa kuna watu wazee, kuna wakina mama na akina baba?

**Audience**: Ndiyo.

**Com. Salome Muigai:** Tuko men and women?

**Audience**: Ndiyo.

**Com. Salome Muigai:** Tunakubaliana tuna watoto, tuna vijana, tuna watu wa kawaida, tuna walemavu kati yetu?

**Audience**: Ndiyo.

**Com. Salome Muigai:** So some of the things tuna consensus tunaka, tunataka nini? Kujadiliana. Ni mambo ya ukweli mtupu kwa hivyo hitaji nafasi ya kujadiliana zaidi. Lakini kuna mambo mengine tunatofatiana. Tuna tofauti ya maoni yangu na maoni yako. Lakini tukisha kubaliana kuwa sisi zote ni Wakenya na tumezungumza sivyo? tutakosana wewe tujuavyo, tutaenda Uganda na mimi nitambaki kuwa Mkenya? Kuna mtu ataenda Tanzania? Kwa hivyo tukisa kubaliana sisi wote ni Wakenya, ni kama watoto wa baba mmoja, nimseme wa mama mmoja, nimseme wa baba na pengine watoto wa baba hatukubaliani kabisa na nyumba moja na nyingine si ni kweli? Ni kweli ama nyinyi Wabukusu na Wakalenjin hamna shida ya mama wa kambo? Mnavyo hizo shida? Lakini kuna wakati mambo ikifikilia na hiyo jamaa ina shida yenye tusahau wale ni wa Nafula, na wewe mama yako anapendwa na wewe mama yako … tunakubaliana sisi sote zote ni watoto wa Mzee wafula. Ni kweli ama sisi zote ni wa Mzee Kibor? Na kazi yetu sasa ni kujadiliana vile tumendesha za mambo yetu, ni kweli hiyo?

Basi sasa wakati huu ni kukubaliana sisi wote ni Wakenya na ni wakati wa kuzungumzia Katiba yetu. Tukisha kubaliana basi hayo, with that brief introduction ningetaka mfungue kitabu yetu cha Katiba. Kwanza niwaeleze kuwa hii ina sura kumi na nane eighteen chapters. Hilo ndiyo jambo la kwanza, na kaba hatujaanza campaign kwenye tulienda wakatwambia Katiba yetu ya

wakati huu haina utangulizi. Haiyelezi ni akina kama Wakenya, kwa hivyo tungetaka Katiba ile tutatengeneza nyingine iwe na utangulizi utweleze sisi ni akina nani yaani Preamble. Basi twasema hii Katiba ilianza na Preamble, na zote tumekubaliana kuwa : "Aware our ethnic, cultural and religious, we the people of Kenya sisi akina nani?

**Audience:** Sisi watu wa Kenya.

**Com. Salome Muigai:** Aware of our ethnic, cultural and religious diversity and determined to live in peace and unity as one indivisible sovereign nation. Ati kuwa tumekubaliana kuwa ni wakabila tofauti, sisi tuna utamaduni tofauti, tuna dini tofauti lakini zaidi ya hizi tumekubaliana kukaa kwa amani, tumekubaliana kukaa kwa, unity ni nini?

**Audience**: Umoja.

**Com. Salome Muigai:** Umoja, tumekubalina kuwa kitu kimoja kisichoweza kugawanywa. Tumekubaliana kuwa taifa moja liloweza kufanya nini? Kugawanywa. Pia tunasema: We are committed to nurturing and protecting the wellbeing of the individual, the family and the community within our nation. Kuwa tumekubalina kufanya nini? Kuifanya nini? Nurturing is to do what? Kulea, na kufanya nini tena? Kuilinda na kufanya nini? Well being maslahi kila siku na Inspector anatueleza habari ya maslahi. Maslahi ya kila mmoja. Iwe ni ya binafsi, iwe ni ya jamaa ama ya jamii kwenye hii taifa letu. Tumekubaliana hayo? Kuna mtu ana swali juu ya hiyo? Nanaana maoni tofauti? Kuna mtu ana maoni tofauti juu ya hiyo? Kuwa hatutaki kuelea, hatuaki kuishi pamoja , hatutaki kuangalia maslahi ya kila mtu? Watu hawataki kuangalia masilahi ya jamii na jamaa pia tukiwa taifa moja?

Basi halafu we recognize the aspirations of our women and men for a government based on the essential values of freedom, democracy, social justice and the rule of law. Nani anataka kututafsiri hiyo? …..(laughter). Kibet inaendelea kua karibu, karibu na Coast.

Recognizing tukitambua aspirations, aspirations ni nini? Matarajio ya akina nani?

**Audience:** Ya wanawake na wanaume.

**Com. Salome Muigai:** Ya wanawake na wanaume. Wakati mwingine tukisema kama tunafikilia mama ni yule mwenye amezaa? Ama ana mtoto, tufikirie pia tunasema wanawake na nani? Na wanaume. For a government based on the essential values. Kwa Serikali iliyo fanya nini? Yenye msingi kuna wamama wanajua Kiswahili hapa kalikali sana. Yenye msingi katika nini? Values kwanza, values ni nini? Ni dhamana zetu, watu wasio na dhamana hawajidhamini. Si ni kweli. If we don't have value then we value ourselves, tuna dhamana na tunajidhamini. Na dhamana zetu ni vipi. Ya kwanza uhuru, ya pili, demokrasia, ya tatu, haki za jamii and rule of law utawala, wenye kisheria.

Exercising our sovereign and inalienable right to determine the form of governance of our country and having fully participated in the Constitution making process. Exercising in kufanya nini? Exercising our sovereign and inalienable right. Kutengeneza haki yetu ya kimsingi ya kufanya nini? Determination to determine the form of governance ya uphold, Serikali yetu, ya nchi yetu, and having fully participated in the Constitution making process. Na baada ya kushiriki kwenye ufujaji wa Katiba yetu do a job and enhance and give to ourselves any of our future generation in this Constitution. Do a job tunapokea ama nini tena? Tumekubali, tumepewa, na give to ourselves na tunajifanya nini? Tunajipatia. Nani anatupatia? Sisi wenyewe tutajipatia and to our future generation tutajipatia sisi na tutasikia kujihadhari people. Tunajipatia nini? Hii Katiba, na tunasema God bless Kenya. Na tunasema kufanya nini? Abariki Kenya. Si nyinyi ni jaribiu nzuri la Kiswahili? Hapa kuna waalimu? Kuna waalimu hapa? Mnaona darasa nzuri ya Kiswahili kuliko nini? Hiyo nilikuwa nataka twende pamoja ndiyo wakati tunawaeleza watu hii Katiba ina msingi gani utaweza kueleza kuwa hii Katiba sisi wenyewe tunazifanya nini? Tunajifugia na tunajipikia. Kwa hivyo hii ni Katiba ya nani, tukikubaliana ni Katiba ya nani? Nani ataitetea?

**Audience**: Sisi.

**Com. Salome Muigai:** Nani atailinda?

**Audience**: Sisi.

**Com. Salome Muigai:** Ikihitaji kubadilishwa nani atabadilisha?

**Audience**: Sisi.

**Com. Salome Muigai:** Tuendelee, nimesema tuna sura kumi nane kwa hii Constitution ama kwa hii Katiba. Hatutaenda moja kwa moja lakini tutaeleza kuwa sura ya kwanza itaeleza kuwa sisi we are sovereignity of the people and the supremacy of the Constitution. Kuwa sisi ni watu wenye kujifanya nini? kujitawala. We are a sovereign people kwa hivyo sisi wenyewe tunajitawala. Na tumeekea nini muhimu? Tumeekea umuhimu

**Audience**: Watu.

**Com. Salome Muigai:** Tumeekea umuhimu watu. Najua wenyewe wameweka muhimu kwa nini? Supremacy of the Constitution. Kwa hivyo tumewekea nini umuhimu?

**Audience**: Sisi wenyewe.

**Com. Salome Muigai:** Sisi watu wenye kujitawala tumewekea nini umuhimu wetu?

**Audience**: Katiba.

**Com. Salome Muigai:** Katiba yetu. Sasa hiyo ndiyo chapter ya kwanza. Chapter ya kwanza inaeleza kinaganaga inafungulia hayo mambo. Inasema sisi ni watu wenye kujitawala na wekea umuhimu ile mkubwa kabisa kwenye Katiba, inaeleza vile tutaweza ku-enforce hii Katiba, tutaweza kutekelezaji na kuhakikisha kuwa inaendelea vizuri pia inasema habari ya kulinda nini? Katiba na pia itazungumzia habari ya sheria za watu za Uganda? Za Tanzania?

**Audience**: Za Kenya.

**Com. Salome Muigai:** Za Kenya. Sura ya pili inatueleza juu ya kuwa sisi nini? The Republic. Sisi nini?

**Audience**: Jamhuri

**Com. Salome Muigai:** Sisi ni Jamhuri. Kwa hivyo ya kwanza ni ya kutueleza Declaration of the Republic, sisi wenyewe tunajitangazia nini? Jamhuri yetu, tunaeleza mipaka yetu, hii Jamhuri ni kutoka wapi mpaka wapi? Tunaelezea nini tena? Capital mji mkuu wetu uko wapi? Tunaelezea pia lugha zetu. Hiyo lugha ndiyo tutazungumzia kidogo. Kuwa tumesema lugha zetu kwetu ni lugha mbili. Lugha rasmi itakuwa lugha ya Kingereza na lugha ya Kiswahili. Lakini lugha yetu ya taifa ni nini? Ni lugha ya Kiswahili.

**Audience:** Lugha ya Kiswahili.

**Com. Salome Muigai:** Pia kitambo tumesema kuwa tutaweza kusaidia lugha zingine. Sio kusema kuwa tutazungumzia Kiswahili ziacha lugha za mama na baba na shangazi. Kuna wakati mwingine shangazi anakuja na lugha tofauti kuliko ile baba na ya mama. Na baba pia na mama wanakua na lugha ya tofauti kwani wakati tuna lugha pia ya kuzungumzia tunazingatia lugha ya baba na ya mama ya shangazi na yote mwingine mwenye iko karibu na sisi tutazingatia hizo lakini lugha zetu za kutumia itakua lugha ngapi ni mbili na lugha ya taifa moja hizo mbili rasmi.

Tunasema kuwa tumezungumzia kuwa sisi kama taifa habari ya dini. Na tumesema je? Tumesema sisi kama taifa …. (inaudible)? Lakini wana taifa wana dini tofauti. Na hizo dini kila dini ya mtu itawekewa manani na itakuwa kwenye usawa na dini ya mwenzake. Tunaelewa hapo?

Tumesema pia kuwa tuna mambo ya national symbols. Symbols ni kitu gani? Ni alama zetu za Kitaifa sivyo. Tusema na alama za kitaifa tutakuwa na gani? Tutakuwa na bendera yetu na nini tena? Tutakuwa na wimbo wa taifa. Ziko hapo angalia kwenye hii mwaalimu ndiyo akukubaliza kuangalia kitabu wakati unayosoma. Wimbo wa taifa na bendera yetu itakuwa ni nini? Ni alama zetu za taifa letu. Na ukiweza utaendelea kutizama part ingine. Tafadhali tunapitia tu hatusomi neno kwa neno, tukifanya

hivi itatuchukua miaka tatu tutatoka hapa na degree. Lakini leo tuna masaa hapa nataka kuwaelekeza vile nimesema.

Halafu pia tuna national oaths and affirmations. Watu wenye tutakawapatia wathifa wa kufikilia jukumu mbalimbali tutawaapisha je? Tumekubaliana hapa waapisha. Kuna watu wengine wajaona hapa kwa kiapo, kuna ajili wengine wetu kwa ajili ya dini ama tofauti fulani hatuwapi. Lakini tunakubaliana so we have the oath and we have affirmations. Tuna makubaliano na tuna kiapo, tumeweka pia hiyo kwenye Katiba yetu.

Pia tumekubaliana kuwa tutakuwa na siku za taifa. Na kwenye hii Katiba tumekuwa na siku chache sana. Utaziangalia hizo, ukikubaliana nazo tutakubaliana, utatuambia zenye ungetaka tutoe ama ungetaka kuongeza. Hiyo ilikuwa sura ya kwanza na ya pili. Sasa twende kwa sura ya tatu.

Sura ya tatu inatuwezesha juu ya pengine na tafuta Kiswahili kwenye, usaidizi wa Kiswahili kwenye maandiko mengine. National goals, values and principles. Nimepatiwa kijikaratasi chenye kuniambia kuwa hii ni kazi tu kuongoza tu shela na doda. Pengine Kiswahili kinakuwa kizito kuliko Kingereza sivyo. Hiyo maswali ya Kiswahili hatusaidii imekuwa zito sana. Lakini maana yake ni mwelekeo wetu. Sisi tunataka kuwelekea wapi kama taifa. Tulikuwa tumezungumzia habari za dhamana yetu, si ni kweli the values. Na sasa tutaongezea nini? Lengo zetu – goals. Goals ni lengo na principles nini?

**Audience**: Msimamo.

**Com. Salome Muigai :** Msimamo? Okay. Sasa tumeongezea kuwa tuna malengo yetu, tuna maana yetu na tuna msimamo wetu kama nini? Kama taifa moja. Pia hiyo mtatazama na mtaona mambo gani tumekubaliana kuwa hayo ndiyo matakwa, lengo letu. Mkinipa dakika moja nitatafuta ………….. (inaudible). Huyu ni mwalimu mwenye makaratasi mengi leo.

Kwa haya lengo yetu dhamana na msimamo …………… (inaudible) – the national goals that is principles contained in this chapter applies to the executive, to the Parliament the Judiciary, local authorities, and all other supreme organs and officials, citizens and prime bodies whenever any of them: applies that is applicable Constitution or any other law and if applies to make and increment policy decisions. Tunasema je? Tunasema haya lengo letu lenye tutakubaliana hizi dhamana zetu, huo msimamo wetu utahusiana nani? Utahusiana kila mtu mwenye ako Kenya ama yeye ni President ama ni mbunge iwe ni mahakama, awe ni wewe mwenyewe,ni …….. (inaudible) ama nini, ama iwe ni kikundi cha watu wenye wameungana pamoja. Tunaelewa?

Yaani one tukisha kubaliana hiyo ndiyo dhamana zetu, mwingine hatakuja kesho atueleze, lakini najua nini ni wa dini wa Kikatoleki. Ninasema tunaelewa? Mwingine hatakuja atuambie mimi utamuduni wetu wa Kikuyu unasema wakina mama watakata masikio ya kondoo peke yake. Kwa hivyo lazima tukataye na pia Katiba ifanye nini? Imesema. Tukikubaliana kuwa sisi ndiyo dhamana zetu tuzazifanyia na tutazirudia kila mara wakati sisi wenyewe tutaishi kwenye hili taifa, na kuona kama umepotea kidogo mzee. Na staki tutumie wakati wote kwa kutafuta hizi makaratasi, nataka tutumie wakati mwingi kwa kuzikiliza. Kwani karatasi tutaenda nayo nyumbani?

Hiyo mwishoni tuna duties of a citizen. Ukiwa wewe una uhuru, hakuna uhuru usio na nini?. Every freedom has got a what?

**Audience**: Limitation.

**Com. Salome Muigai:** Has got a limitation and what else? A responsibility that is it. Kuna uhuru wenye huna jukumu? Ukiwa wewe ni …………. (inaudible) useme hapa ni kwangu ni lazima wezi wakipiga mlango ukuwe wa kwanza kufanya nini? Kwenda kwa mlango, huwezi kwenda chini ya kitanda. Mwanzo wewe utakuwako hiyo ni uhuru ni lazima uwe na nini? Na jukumu. Kwa hivyo sisi Wanakenya tumepatiwa haki zetu na tutaangalia haki zenye tumetupatiwa na uhuru mwenye tumepatiwa. Kwa hivyo pia tutaangalia tuna jukumu zipi. Hizi jukumu zinasema hivi:

"Inorder to fulfil the national goals values and principles all citizens have the duty, kila mwananchi ana jukumu la kufanya hivi. Aquaint themselves with the provisions of the Constitution and to propagate its ideals and objectives. Afanye nini? Ajijiulishe yeye wenyewe matakwa ya juu ya Katiba na akisha jua afanye nini? Aendeleze na apeleke wengine. Hilo ni jukum katika Constitution, Katiba mpya. And uphold and defend the Constitution. Afanye nini? Yeye mwenyewe awekee maanani lakini hiyo pia haitoshi lazima ufanye nini pia? Lazima uilinde hii Katiba. Exercise ya democratic rights by voting and being involved in other forms of political participation. Lazima afanye nini ukiwa wewe ni mwana Kenya? Uendeleze haki zako za kidemokasia kwa kufanya nini? Kwa kupiga kura. Na kujihuziza katika mambo ya nini? Ya siasa. Napenda neno siasa kwa Kiswahili. Ama pia kwa Kiswahili na kwa Kingereza, siasa ndiyo huleta sela. Mnajua sera ni nini? Politics is what produces policies and twe all live under politics, don't we? Tuna policy ya juu nini kwa mfano. Tuna policy ya masomo, tuna quality ya nini?

**Audience**: ya elimu.

**Com. Salome Muigai:** Ya elimu. ya nini nyingine?

**Audience**: Ya utawala.

**Com. Salome Muigai:** Ya utawala. Na policy ya nini tena?

**Audience**:……………… (inaudible)

**Com. Salome Muigai:** Ya afya, ya chakula, ya chochote kile sharti tuwe na policy ya kumpua. Tuna policy ya kumpua? Lazima tuwe nayo. Tuna policy ya mazingara, na mazingara ndiyo inatupa nini? Ile oxygen yenyewe tunapumua sivyo? Basi tulipokuwa na policy nzuri ya mazingara siku moja tutakosa hewa yanyewe ya kumpumua. Siku moja tutakosha maji? Kwa hivyo lazima tuwe na sera ya nini? Ya mazingara ndiyo tupumue sivyo? So we need kila mtu lazima ajifundishe na siasa ndiyo

tuwe na sera nzuri. Hiyo ndiyo ile Katiba ya leo inavyoeleza, na hiyo inasema kuwa engage in work including home making for the support and welfare of the self and their families, for the common good and contribute to the national development.

Wakati wa kusema kazi ni nyingi. Kazi ni nini?

**Audience:** Ni uhai.

**Com. Salome Muigai:** Kazi ni uhai. Kazi ni utu. Ukiwa wewe ni mwanadamu na hufanyi kazi wewe sio mtu, sababu yale mambo yote mengine tunafanya wanyama pia wanafanya. Wanyama wanakula? Wanapumua? Wanapata watoto? Kwa hivyo tofauti yetu na wanyama ni kuwa tunafanya nini?

**Audience:** Tunafanya kazi.

**Com. Salome Muigai:** Tunafanya kazi. Kazi ni utu. Kwa hivyo hii Katiba ya leo inatueleza ni lazima tufanye kazi kwa maslahi ya nani?

**Audience:** Yetu.

**Com. Salome Muigai:** Yangu mimi mwenyewe mwanzo, ya familia yangu, na ya jamaa na nini? Na taifa nzima. Na hayo matakwa mengine ya jukumu za wananchi wa Kenya unaweza kujisomea mwenyewe nyumbani.

Leo tuna uhuru wa afya ya kutosha. Haza waalimu wenye wako nyumbani leo tunawapa homework na kila mtu. Tafadhalai tuendelee kuisoma hiyo tuone inatueleza nini.

Halafu tuendelea kwa chapter, sura ya nne. Sura ya nne ni uwananchi, citizenship. Inatueleza kwanza kwa kinaganaga general principles, msimamo wetu kuhusu uwananchi yaani general principles concerning citizenship.

Halafu inatwambia ile tunaweza kufanya, limitations. Kudumisha, that's good, mimi sijaona watu wenye wanajua Kiswahili kama wananchi. Vile tunaweza kudumisha uwananchi wenye tayari tunayo. Halafu pia tinatueleza vile tunaweza kumpata wananchi kama hatuko nayo tayari. Inatueleza tuna wananchi wa kuadilia kufanya nini? Ya kuzaliwa, kuleta wananchi kwa kufanya nini. Bado we niangalilie moja kwa moja tufuate utaratibu uliokuja hapa. Wananchi kwa kuzaliwa , wapili nini? Kuandikisha, wa tatu, kuna ufananichi wa kuolewa na kuoa. Hiyo ilikuwa kikao. Zamani hata kwa kanisa yenye iko wakati huu mwamume akimuoa bibi asiye Mkenya anakwenda kumpa uwananchi. Lakini mama mwanamke akiolewa na mtu asiye Mkenya hana hati ya kumpa uwananchi. Sasa hii Katiba mpya inasema kuwa: "ukioa au uolewa na Mkenya una haki ya nini? Ya kuwa ya uwananchi. Hiyo ya kuoa na kuolewa haikuwa shida kubwa. Shida kubwa ilikuwa hii mzee alienda kusoma

ngambo, mchana ameolewa na mzungu, amekaa huko miaka ishirini, mzee mgonjwa yuko kitandani, watoto wote wanakuja kufanya nini? Kumuona. Mama anafika Airport na watoto wake mpaka mjukuu mwenye ameitwa jina ya babu kuwa ni Mbukusu na haiti jina la mwenye babu hajafariki siku hizi naona tunabadilisha, na wengine halafu mama anaambiwa wewe ingia wewe ni nini? Ni mwananchi. Lakini wale watoto wako sio nini?

**Audience**: Wakenya.

**Com. Salome Muigai:** Sio Wakenya. Warudi kwao. Wakiwa hawana visa wafanye nini? Warudi kwao. Mzee bado yuko Kenyatta National Hospital kitu moja kimemweka asiingie kwenye amegonga kule mlangoni mbinguni ni kitu gani? Ni kuona nini wajukuu. Nao wajukuu wamekatazwa kufanya nini, kuingia. Kwa hivyo tunasema kuwa mtoto wote aliyezaliwa na mzazi mmoja Mkenya na huyo mtoto ni niece hiyo mtoto ni nani? Ni Mkenya. Ikiwa mzazi mmoja ni Mkenya huyo mtoto ni Mkenya. Hiyo ndio moja tulisikia tumeongeza. Watu wengi sana watwambia kuwa pia wakitaka kuwa wananchi wa nchi zaidi ya moja tukumbalishe watu wakuwe wananchi wa nchi mbili. Watu gani walitwambia? Tuliambiwa na jamii ya wabukusu wenye kukaa karibu na Lwakhakha wanasema hawa ni Wa………….. tafadhali tukubalieni tuwe upande huu ama upande ule mwingine.

Pia tuliambiwa na jamii ya Kiteso. Walituambia sisi tuko upande huu na upande ule. Tuliambiwa pia na Wasamia na watu wengine wenye wako Busia na upande huo. Na hivi sasa tuliambiwa pia Mandera na wananchi wa Kisomali. Wasema sisi hapa ni pahali pa ukavu kubwa, wakati tunakua hapa kuna kiangazi kubwa hapa Kenya sisi tunachukua gamia zetu twapeleka wapi? Somabra ndivyo tuseweze kusikia kukufa na mifugo yetu na mbuzi zetu. Somalia kukiwa hakuna mvua tunavyochukuwa tunapeleka wapi? Ethiopia. Tafadhali tukumbalisheni sisi tuwe wananchi wa nchi moja ama nyingine kwa wakati mmoja. Kwani ukweli wa mambo vile tunavyoishi ni kusema sisi tunaenda kule na kurundi huku na ni lazima tufanye nini tukiwa twaweza kuendelesha maisha yetu ya maisha ya mifugo yetu. Kwa hivyo kwa nini Katiba tumependekeza kuwa wananchi wakumbalishwe kua na dual citizenship.

Halafu pia tuzungumzie pahali tutakaipoteza uwananchi wetu, utafanya nini ndiyo upoteza kuwa wananchi. Na pia nimesema kuwa watoto akiachwa na baba kabla hajaliwa na pengine baba amekuwa amemuacha huyo mtoto kwa tume ya mama huyo mama na mtoto wakiwa America , huyo mtoto ni Mkenya? Tumesema nini huyu mtoto tayari amezakuwa mtu na huyu mtu wa watu, tumezungumshia pia habari ya kuishi kuwa Wakenya hatapewa hatazanganywa uwanchi kwa ajili ya kule ana kaa tumezungumzia habari ya uwezo tuliyopatia bunge kuhusu wananchi waliyotangalia pale, na pia tulizungumshia habari citizenship registration for tumeweka kikao pale cha kufikilia habari ya uwananchi wa Kenya.

Sasa twende kwa chapter ya sura ya tano. Kwenye haki za binadamu the Bill of Rights kwanza tumezungumshia habari za fundamental rights and freedoms. Haki za kimsingi tumesema kuwa haki za kimsingi humpatiwi na mtu. Hupatiwi na Serikali, hupatiwi na yeyote ile. Hii hi haki unayozaliwa nayo kwa kuwa wewe ni nani? Ni mwanadamu, end of story. Nilikuwa

sijapatiwa kitu chochote naweza kukupokonya? Naweza kukupokonya kiasi nisikukupatia nikiwa mimi si mwizi? Na Katiba sio hali ya uwizi. Kwa hivyo tunasema si haki kwani hukupatiwa na yeyote huwezi kupokonywa na nani? Na yeyote. Ni zako na lazima ziheshimiwe.

Tunasema kuwa pia nchi, State, Serikali, Serikali sio state, state ni nini. Ni taifa. Taifa lina jukumu kukuhakikishia haki zako. Kwa hivyo utasoma provisions zenye tumepeana kwendeleza hayo. Tumesema pia kuwa haki zako zina kikomo. Kuna mwanatume mmoja mwezangu anaitwa Lethome alisomea hata uwakili Pakistan wakati alikuwa amesaandika Katiba yao. Kwa hivyo watu wa Pakistan walikuwa wanasikia wananguvu sana kwa ajili ya Katiba mpya. Walikuwa wakitembea wakitupa mikono yao. One … two. Halafu kumbe yeye alitupa yake kwa ajili ya utu wake ……….. (ainaudible) na mwingine. Kwa hivyo kitu cha kwanza cha kulekebisha kwenye Katiba yake ni kusema kuwa haki yako inakushia pahali yangu uaenda. Kwa hivyo haki kutupa mikono wako utakuishia pahali lako, kwa langu nafanya nini? Kwa hivyo hakuna haki zenye hakina kikomo na kusoma na kuonyeshe vile sheria zimepelekwa hapo utaonyeshwa haki zetu zina kikomo kipi?

Tumezungumzia kuwa kuna haki ya uhai, ya kulingana na hiyo tumeondolewa mbali adhabu ya kifo tumesema uhai upatiwangwe na Mungu na ni Mungu tu mwenye anaweza nini? Kuondoa.

Tunasema kuna haki kuna usawa kwenye Katiba, uswa wa kila mtu kwenye Katiba. usawa kila mtu. Ukiwa wewe ni Mkenya unasawa moja na Mkenya mwezako. Tumesema pia una haki ya kutoka ku-discrimination, kubaguliwa. Katiba haijakubalisha ubaguliwe au ubaguliwe kwa kuwa mweusi kuliko watu wale wengine au kwa kuwa mwekundu kwa kuwa mlemavu, kwa kuwa mwanamke, kwa kuwa chochote kile na cha mambo vile Katiba haitakubaliza kubaguliwa juu ya yayo.

Tunasema kwenya Katiba hii mpya haki za wanawake na tumelezwa kwa kilefu kwenye hiyo Katiba tumesema kuna haki la wazee wakongwe. Hii Katiba ya leo imewapa wazee haki za namna mbali mbali.

Pia kuna haki za watoto. Jamii isiyochunga watoto wao haina nini? Jamii isiyochunga watoto yao haina nini? Haina usoni. Ni kama mkulima mwenye habari. Unaweza kuwa mkulima na wakati mvua imenyesha hupandi. Na kwa hivyo na ukipanda lazima uangaliwe hizo mbegu, lazima tubadilize, lazima tufanye nini na machine hapa ni pahali ya wakulima. Ukisa panda mahindi unayafanya nini? Unapanda hizo ukifanya nini tena? Unapalilia na kukula tu basi mara moja hiyo. Unaweka mbolea unafanya nini?

**Audience**: Unaweka bolea.

**Com. Salome Muigai:** Unaweka mbolea unafanya nini tena? Unaweka dawa na mambo mengi kama hayo. Si ni ukweli? Basi jamii hii ya Kenya imekubaliana kuchunga watoto wake.

Kuna haki cha ya kifamilia. Majengo ya – hili jengo limejengwa kwa nini? Tumetumiaa nini kujenga hii nyumba? Tumetumia mawe. Kanisa limejengwa na nini? Mawe ya kujenga taifa ni nini?

**Audience**: Raia.

**Com. Salome Muigai:** Na jengo moja na raia unajua hata ni nini? Hii jiwe ndani yake inatumika ina nini ni lazima iwekwe hiyo ndilo liwe jiwe. Likuwe block, sivyo? Na block ya kujenga taifa ni nini? Tujaliwe. Kwa hivyo sisi wenye Katiba tumeangalia haki za familia yetu ama jamii.

Tumeangalia pia haki za watu wenye ulemavu. Tumesema watu wenye ulemavu wana haki zao. Ni lazima tukifanya mjengo wetu tukubali tukumbuke tuna watu kama hao na lazima tukiwa kwenye jamii na tuwe na hao watoto wapewe nafasi yao na lazima shule zetu zikumbuke kuna watu kama hao na watoto wetu ikiwezekana wale walio na ulemavu na wasio na walemavu wasemekane ni watu wa shule pamoja. Tunataka wafanye nini? Wasome pamoja wajuane. Watu kufanya nini? Ni kujuana na kujua na akafanya nini?

**Audience**: Aakudhamini.

**Com. Salome Muigai:** Akudhamini. Tuna haki – tumezungumzia habari ya haki ya utu wa mtu. Human diginity. Utu huo lazima upewe heshima na hizo heshima zake zimekuwa kwenye Katiba hii mpya.

Tumefikiria habari ya uhuru na nini? Security na usalama wa kila mtu kwenye hii Katiba. tumefikilia kuwa lazima mtu kila mtu alindwe kutokana na utumwa, kutokana na kufanya kazi bila mshahara na kutokana na kufanya kazi kwa nguvu. We are protecting our citizenry from slavery servitude, and forced labour. Tunataka kila mtu akuwe na privacy akuwe na nini kwa Kiswahili?

**Audience**: …………….. (inaudible)

**Com. Salome Muigai** : Ushindi, faraja, basi tunaelewana hivyo kuwa heshima yangu isingiliwe ovyo ovyo bila mimi kujua bila watu kupata afya ya kufanya hivyo. Kwa kuwa we want your privacy to be protected.

Tuna haki ya kuabudu na kuamini, na ya kueleza hiyo kwamini kwetu – freedom of religion, belief and opinion. Tuna haki ya kujieleza freedom of expression, participation au tuna haki ya kuandikisha hiyo opinion nini? Maoni yangu, tuna haki ya kupata habari – right to information, tuna haki ya kumpata habari driving information, tuna haki za kupata habari, pia vile zinafanyika, tuna haki ya kukutana pamoja, freedom of association, tuna haki ya ku-attempt demonstration, picketing, na petition, tuna haki

kukutana na kuandamana mradi tu uwe?

**Audience**: Amani.

**Com. Salome Muigai:** Kwa amani. Tuna haki za kisiasa, tuna uhuru wa kutembea kila pahali katika nchi na kufanya nini?

**Audience:** kuishi pahali popote.

**Com. Salome Muigai:** Na kuishi pahali popote pale, kuna haki za wakimbizi- Refugees and asylum seekers. Yule mtu mwenye atakimbia akuje kwetu, tuna haki, ana haki zake.

Tuna uhuru wa kufanya biashara, wa kupata kazi, na wakufanya nini, freedom of trade, wa kupata kazi, na kufanya nini – Freedom of trade, occupation and profession. Uhuru wa biashara, hiyo sio ukazi occupation ni kama kazi, na profession, utala. Kufanya kazi ya kitala.

Tumezungumshia habari za uhuru wa kuwa na property, na kuwa na mali. Uhuru wa labour relationship, ushilikiano katika kufanya kazi, social security hiyo ni nini? Kila mtu hapa analipa social security fund. Tunaita je kwa Kiswahili? Ni kuwa na pesa ile inaweza kukulinda wakati wa taabu. Sivyo?

Na pia tuna haki ya afya,haki ya elimu, haki ya kuwa na nyumba, haki ya kuwa chakula, haki maji, na haki ya sanitation, haki ya usafi, ubora pia.

Tuna haki za mazingira, tuna haki ya lugha na utamaduni, kuna haki consumer rights, ya ununuzi sivyo. Huwa ni mtu na haki zako, tuna haki kupata fair administration, tuna haki ya kuwa na utawala bora, siyo kuwa kwa utawala, ni kuwa utawala nini?

**Audience**: bora.

**Com. Salome Muigai:** Tuna haki not to obey unlawful instructions, hiyo ni haki ya nini?

**Audience**: Ya kutotii sheria.

**Com. Salome Muigai:** Ya kutoti sheria zizo za haki. Mtu akwachia uuwe fulani, anajiimiza. Hiyo ni sheria kweli umeambiwa na mkubwa lakini sheria ya kweli ni ya haki?

Tuna haki kwesha kufanya kufikia kortoni. Access to court, haki ya kufika kortini. Just one thing Sasia yuko hapa? Sasia wapi ni nini duty unapeleka kwa Braille. Umeleta ?

**Sasia**: Hapana.

**Com. Salome Muigai:** …………. (inaudible) umesapata hizo habari za Braille? Lakini sio ile nasoma wakati huu. Ina haki za walemavu, na haki zingine zote zinazo wahusu ulemavu. Lakini hiyo pia ni mwanzo ya – that is the first step, the latter hii joblet ikiwa kwenye Braille, lakini kwa wakati huu tume aanza hiyo.

Tuna haki wenye wamefanya nini. Wameshikwa. Ukiwa wewe umeshikwa una haki zako, tuna haki za kufanyiwa fair trial. Kua na nini?

**Audience**: Haki ya kujitetea.

**Com. Salome Muigai** : Fair trial ni haki ya kufanya nini? Kuhukumiwa kwa haki. Hata kabla ya kuhukumiwa tutafanya nini kwanza? Una haki ya kuzikishwa, una haki ya kufanyiwa kesi iliyo nini? Iliyo na haki. Sivyo. Kuna haki ya mshikiwa mwenye tayari amesha wekwa kuzuizi. Wakati wa what is State of Emergency?

**Audience:** hali ya hatari.

**Com. Salome Muigai:** Wakati wa hali ya hatari, pia tumewangalia. Kutakuwa na uhusiano gani haki zako wakati wa hatari? Tunaangalia pia Rights to ask the Commission on Human Rights and Administrative Justice or court to uphold the Bill of Rights. Wakati haki zangu zimetatizwa, tutaweka tume yenye inaweza kwenda kuyandia iangaliwe zote haki zangu. There will be a Commission yenye itangalia hizo Commissions nyumaye.

Authority of the court to uphold and enforce the Bill of Rights. Haki ya court kuangalia nini? Kuangalia kuwa haki zangu hazijatatishwa. Interpretation of the Bills of Rights vile itakavyoangaliwa. Tukisema haki za maana gani? Utafikiri, hiyo tumeendelea kila pahali lakini kwa yenye tumembakisha sasa kubaliana na mimi hatujaenda bila tujengewe. Lakini hiyo ya haki kwani kila pahali yenye tulienda kwa razima kuwe na shida na haki zao na haki zao na vile walifikilia zimetwa ndiyo zimenda kitengele kwa kitengele.

Lakini sasa tukienda kwa chapter six sura ya sita, representation of the People, uwakilishi wa watu, tunasema kuwa kuna general principles, kuna maoni ya nini?

**Audience**: Ya jumala,

**Com. Salome Muigai:** Ya jumla asante, maoni ya jumla, kuna habari mpya hapa election ni nini?

**Audience**: Upigaji kura.

**Com. Salome Muigai:** Upigaji kura, kuna haki, the right to vote, haki ya kufanya, haki ya nini? Kupiga kura, qualification for registration nini hiyo? Kuhitimu kujiandikisha, kutohitimu kujiandikisha, ama kuandikishwa, voting. Tumezungumzia habari ya upigaji wa kura, na vile tutakavyofanya na unopposed candidates.

Ningetaka kueleezea vipengele visili sisi hapo. Kwanza ni ile ya Election. Wakati tulipokwenda kusikiliza wananchi kuna mambo mawili yenye tuliambiwa, pahali yenye watu wengi kama tunayo Transnzoia, Central Province, penye watu wengi, Western Province, tumeambiwa kuwa lazima kile kikao cha bunge kilinganizwe na watu wenye kukaa hapo.

Population: ni lazima kila constituency ilingane na population. Tulipoenda Mandera na Wajir na Kajiado na Transmara, tuliambiwa kuwa kwetu watu wako mbali sana moja kwa mwingine. Kwa hivyo mkisema watu wa kikao cha bunge kilinganishwe na population, mimi nitakaa miaka ishirini sijaona mbunge wangu. Kutoka kuzaliwa nitamalize shule, atakwenda kufanya kazi hajamuona mbunge. Kwani wakati wengine inatubidi kwenda maili mia tano ndiyo tufikie pahali twenye tunaweza kuona nyinyi. Sio ni mtu ako na haki zake? Zio yote ni kweli? Sasa wewe ungekuwa huko ungechukua nini? Ungechukua wenye walikwambia uangalia population, uangalia wingi wa watu, ama ungechukua hua nafasi za kutembea ni mbali na hata barabara hawana? Ungechukuliwa gani maana yake?

**Audience:** …………….. (inaudible)

**Com. Salome Muigai:** Sisi wenye tume tulichukulia yote mawili, tukasema hawa wenye kutembea mbali mbali ni Wakenya, hawa wenye wingi ni Wakenya. Kwa hivyo tukafikilia tunaweza kuangalia vile watu wanaweza kusaidika, na ndiyo tumebakisha kidogo hali ya upigaji wa kura. Tumesema hivyo. Kawaida hapa Kenya kupita kura mtu mwenye kupata kura nyingi ndiyo umepata kujisifu. Lakini wakati ujao tutapiga kura mara mbili. Utapigia mbunge wako, ndiyo utapigia chama. Itakuwa fracas kwa mbunge. Mzee leo wakati huu tuko kwa programme ya kuskiza. Tupata programme wakati wa kueleza, na tukapata kila wakati ya kuenda nyumbani kufanya homework na kuburudishia Bwana Sasia maoni yetu.

Wakati huu mimi nataka tu kueleza ni watu waelewe tuko wapi, kwani tunasema hivi? Tunasema hivi kwa sababu ikiwa hapa kwa mfano ama tutoke hapa hospitali tufanyie twende nyumbani kidogo. Kama watu wa Eldoret wakikubali wanapigia Bwana Bibi Salome kura. Watanipia kura na mimi niwe nasimama kwa chama kipi? Katiba one. Mimi niko kwa chama cha Katiba one nanapigwa kura. Watapiga kura ya Salome kwa jina na watapiga kura Katiba one. Salome ikiwa ndiyo mwenye alipata kura nyingi ataenda bunge. Kuna watu wenye hawapendi Salome, lakini wanapenda Katiba watu. Kwa hivyo mtu anweza kukosa kupigia Salome na akipigia Katiba. Kwa hivyo tuta hesabu , Salome akisha enda bunge ama akose kuenda tutachukuwa zile board za chama kimechukua. Halafu tutalinganiza na kesi itagawanywa. Kwa hivyo ile chama kile kitakuwa

na wapiga kura wengi zaidi ama kule ndiyo watakuwa nazo, zitagawanywa kwa vile tumekubaliana na wanapata vitu vingine vya zianda.

What does that mean? Ina maana nini? Kukiwa Eldoret kuna watu mia kitu waliyopigia Katiba one na pahali pengine na party zingine zimepigiwa kura ishirini. Ni kusema Katiba one itakuwa na viti vingapi?

Ikiwa viti vya Katiba hii ingine ina kiti kimoja kwa ajili ina kura ishirini, Katiba one inakuwa na viti ngapi? Itakuwa na viti kumi. Kwa sababu unachukua zawadi ni wengi. Kwa hivyo haitakuwa kama mkiwa wengi sasa ndiyo mnaweza kutumia viti zaidi. Mnanielewa? Lakini yule mwenye alikuwa viti zake pale mbali basi hatujamnyanganya kile kiti chake. Yule mtu wa Wajir wenye wakilishi kumi ama ni watu watano basi shikiliano cha watu wangapi tano. Faida gani itakayoletwa na hizi viti. Ikiwa Katiba one walikuwa Salome aingie na sasa amesha ingia sasa wana viti vingine ngapi? Tisa. Kiingine huko kwenye kama hapa ni mchanganyiko wa makabila, Salome ataingia na ni kabila moja, na kumbe tunataka pia kufanya chama chetu kiwe na shule ya kitaifa. Watasema Salome ameingia ni Kikiyu tumemalizana na hiyo kiti ya Wakikuyu lakini bado tuna viti vingine tisa.

Vitatu tutafalia mmoja Kalenjin kwani tuko na vitatu kuingine tutapatia Bukusu ingine tutapatia Mkamba. Ishitoshe kueleza kuwa percentage nchi nzima watataka viti vyao lakini wenye wamechaguliwa wote ni wanaume. Ama wote ni wanawake. Kwa mfano bado saa hii tuna viti vingine tunapatia tunataka wakina nani. Wanyonge kama watu wenye watapitiwa ni party ni wanawake. Pia huu ni wakati wa kusema tumepata watu wetu lakini kati yetu hatuna wakili, hatuna mtu mwenye anaweza kutusaidia kufanya post ya non-chief, yaani wanaweza pia kutumia hicho nafasi kuleta wataalam kwenye uongozi. Waweza pia kufikilia hapa pahali zetu hii ni mbali lakini ni mkali kubwa hapa.

**Audience**: Catholic

**Com. Salome Muigai:** Kwa nini mnataka kusema tunapeleka catholic mmoja? Tunataka tushikiliane na hiyo ni Mungu wenye huru kwenye maendeleo. Ama wataenda kusema tumeleta watu wengi hii programme inatuwezeza kuleta watu wengi kwenye uongozi. Ama tunaweza kusema tuna wazee hapa wana akilizao mzee fulani mtu mwenye akili zake, ni mtu mwenye hekima, ni mtu mwenye anaweza kusaidia hiyo. Laini habari ya campaign atafanya nini? Hataweza. Lakini wakti huu sasa tumepata nafasi ya kumwafikisa nani yule mzee akaleta ile hekima zake kwenye utawala wa hii nchi. ………… (interjection)
Mzee I don't want to take questions right now. Ukinilazimisha uandike nchini nikimaliza, mkija mara moja walk in, walk out, Katiba tunasema ni safari nje, kama hujakuja. Sio habari ya kuingia na kutoka. It is a time to come later season together. kwa hivyo tafadhali mimi nitamalisha kueleezea na mara nyingi kufanya introduction ya hii Katiba mwenye ako na maswali ataniuliza mwishowe.

Nilikuwa ninataka kueleza habari juu ya Election. Zamani nilisema nina ……… (inaudible) viwili zenye nataka kueleza juu ya ile

habari sura hii mjomba tuzikizane. Hii ni safari ndefu tuko kwa sura ya tatu. Na tulisema hii ni ya sura ya kumi nane kwa hivyo tafadhali tuelewane. Ninataka kueleza kidogo juu ya "unopposed candidiates. Kwa katiba yaliyoko sasa mtu akiwa hana upingamizi, hana mtu mwenye anampinga, hapigiwi kura. Tunaweza kusema yeye ameshafanya nini? Amesha faulu. Wakati ujao atafanyiwa kura. Atakuwa yeye peke yake. Kwa sababu gani? Kwa sababu hizi mbili:

Watu wakishampigia kura pia watapitia chama. Okay. Hiyo ni nafasi ya kwanza.
Ya pili utaeleza kwa kinaga ukifika kwa wakati vyama ya siasa. Lakini vyama vya siasa vitakatwa pesa kulingana na kura zake. Kwa hivyo mtafikia kupiga kura kwani ni mtu mzuri sana ndiyo mnataka peke yake mumefanya nini? Munyima chama chake pesa na kura zenye mkijesidia kwa pesa. Kwa hivyo hata ikiwa mtu mmoja ndiyo amesimama bado mtapiga nini? Mtapiga kura. Hiyo ndiyo maneno mawi ndio nilikuwa kueleza kwenye hiyo.

The Electoral Commission: Tumeeleza kuwa tutakuwa na tume mpya ya Electoral Commission, tumekanisha watu wenye walikuwako badaaye watu ishirini na tisa na watu wangapi? Tumesikizisha ama nani? Not to make a deal sio saidi ya ngapi, sio chini ya nane na sio zaidi ya kumi. Hiyo ni tofauti moja.

Tofauti ya pili ni vile wana katiwa uchaguzi unaweza kuyasoma hapo. Lakini kitu moja nataka kusema huu ni kuwa tumesema kuwa tukifanya ile uchaguzi wa kwanza tutakayofanya ni hii Katiba mpya, tutatumia tume ile itakuwa bado iko kwa wakati huo. Tunaelewana. Tukisema hizo cadets itachukua hii Katiba mpya, uchaguzi wa kwanza kwenye hii Katiba mpya tutatumia tume imechagua iko wakati huo. Baada ya kufanyiza hiyo uchaguzi huo, baada ya kisa ile tutawaomba kujiuzuru ndiyo tulete ndiyo tulete tume mpya. Kwa hivyo hatutaki kuenda taafu, hataki kuenda pengo huwa Katiba mpya inataka tume fulani na hiyo tume fulani haiko kwa hivyo hatuwezi kufanya uchaguzi mpaka tume ifanye nini? Iwekwe. Tumenyeta kuwako ndiyo yenye tutafanye nalo uchaguzi wa kwanza wenye Katiba mpya halafu baadaye tutapata tume nyingine. Hiyo ndiyo mambo mawili yenye nataka kuelezea kwenya habari ya tume ya uchaguzi.

Mambo ya yaliyo kitengele ni Political parties. Vyama ya siasa. Mambo matatu tunataka kuelezea juu ya hiyo. Kwanza ni kua tume ya uchaguzi ndiyo yenye itakuwa ikiayajuliza vyama ya siasa kwa Katiba hii kwa mswanda huu wa Katiba.

The Electoral Commission one of the functions ambaye ya kutekeleza uchaguzi itakuwa pia ikisajuliza vyama siasa.

Vyama vya siasa vimesema kuwa vitagewa pesa za taifa. Lakini zitapata pesa kulingana na kura zao. Kwa hivyo chema chenye hakikufikia kura na mtu yeyote nayo kutofia hakuna mtu mwenye atawapatia pesa.

Na jambo la pili litakuwa cheme kienye kuwaleta akina mama pia kitakuwa na nafasi ya kupatiwa pesa ya nchi kidogo. Kwani kuwahusiza akina mama kwenye siasa itakuwa shida moja kubwa kwenye hii taifa.

Mambo ya chama vya siasa ni mengi yene tumezungumshia tumesema lazima ziwe na kali kuwa viama vya kitaifa hatutaki vyama vya kikabila na mambo mengi mengi tumekubaliana vile tutakavyo sajilishwa na pia vile zitaondolewa kwenye badilizo. Zikifanya nini ndio ziondoa. Zitangaliwa nani? What permission is going to be there? Kutakuwa party discipline? Hiyo ni nini?

**Audience**: Nidham,

**Com. Salome Muigai:** Nidham ya vyama vya siasa. Lazima zenyewe ziwe kama mtu wa demokrasia. Kama hakuna demokrasia ndani zitaweza je kuwakisha Serikali yenye nini, yenye demokrasia kwa vile uwezo wake.

Tikiangalia chapter seven ana sura ya saba tunafanya nini pale. Tunaakisha bunge, tunaisemea kazi ya bunge itakuwa gani? tunaipa bunge jukumu mpya na hilo ni la kukumbalia ama kukataa watu wenye wamesa chaguliwa kwa watu mbali mbali katika nchi hii.

Hii ni majina ile tulitoa kwa wananchi walituambia lazima bunge ihushishwe kwani bunge ndiye inasimamia watu. Na lazima ihuzishwe kwenye kuajili watu katika wadhiba tofauti. Pia tumesema ya kuwa ikawa bunge hata budget kwa Katiba iliyoko sasa inarundishwa kwenye budget. Hataki ihuhushizwe tu kukubalia na hiyo budget. Tunataka ihuzishwe kuitengeza hiyo budget. Kwani bunge, mbunge wako ndiye mwenye sauti ya nani? Sauti yangu. Halafu tunatengeneza chini hapo composition of Parliament and Constitution of members. Kwamba hapo nina maneno mawili matatu ningependa kuwalezea. Kwanza ni kuwa tumeweka bunge yenye vibadili, yenye vikao viwili. Kuna kikao cha wabumbe wenye tumewachugua yenye itakuwa ndiyo Parliament ama National Assembly na kuna National Council yenye itakuwa ya wakilishi mmoja kutoka kila wilaya katika Kenya nzima.

Zaidi ya hapo watakuwa wao watafika katibu sabini hivi itakuwa hivi ya wakilishi wengine thelathini wa kike. Kwa hivyo tukipatiwa tukija Rift Valley, tukija Tranzoia, tume number moja tutarudi tena Rift Valley tuwaombe mtupe akina mama wanne. At least 4 x 8 watakuwa wangapi? Thelathini na wawili. Nairobi nafikiri atakuwa mmoja kwa hivyo haitafika. Tunahitaji kuwa na kikao cha bunge chenye theluthi moja itakuwa akina mama. Kw ahivyo hiyo tunaelewa.

Tulizungumshia habari ya kuwa kuna viti za ziada kwenye uchaguzi. Tulikubaliana kuwa wakati chama kimepata kura nyingi kitapatiwa viti vingine vya zianda hivyo. Hamtakubali? Haya mtanizungumsha na mimi kwangu ni kuambia yenye kiko hapa kukubaliana na kutokubaliana ni date ya pili. Najua tuelewe kile kiko hapa na kwa nini kimewekwa hapa halafu tunzungumshie nyumbani tutaenda tutafika pahali njiani. Kwa vile ile duty yenye tutapatiwa vyama vitakuwa viti tisaini za zianda. Hicho viti msiake zitanenda kwa akina mama forty five. Lakini hao wakina mama wakuwa wametoka kwa vyama.

Halafu mnakumbuka siku moja nikija hapa tukanyamaza mtueleze kile mnataka? Tulinyamaza siku mbili hapa mkitueleza? Na mlisema mnaweza kuturundishia hiyo ………… (inaudible) halafu muende mseme twataka nani? Okay. We sat here recently

busy, you said things, we agree some did not agree did anybody take it we did not agree? We listened.

Now I am asking you to do the same. You listen you take notes, what you agree with, you take note what you disagree with but you allow me to say a word a work be. Did we agree on that?

**Audience**: Yes.

**Com. Salome Muigai:** Because if you don't tutakuwa bado tuko kwenye hiyo halafu hatutaelewa nyingine na kisa kuwa nime-sign that. Wengine wataelewa wenye ujuzi wa Katiba, wengine hawatakuwa hawajaelewa kwa hivyo ningetaka kuwauliza na kuwaomba mtu akuwe patient. Katiba debating is a patient process. ………….. (laughter). Tumefika wapi? Tumesema 45 nusu yake iende kwa akina mama. Hii nusu nyingine utakuwa katikati kuna walemavu, katika kutakuwa na wazee, katika kutakuwa na watalaam na watu wetu wengine wenye utaona kuwa tunahitaji wenye sejemu zetu za kufanyia decisions making lakini hawako. Tutahitaji lakini hawafanyi nini? Hawako.

Ukiangalia pia the right party ilikubaliana haki tulikubaliana kuwa kila ……… (inaudible) ana haki wa kujulidishwa in decision making. Kwani mwenye hayuko ……….. (inaudible) je? Asiye kuwako na lake haliko. Kenya hajari mwenye haliko Kenya.

Ogiek wanamalisha miaka ngapi ndiyo waweze mjumbe kwenye bunge kwa kura? Kwa hivyo tunasema tutii Katiba imsimamie iliye party yake mbilo lenye litamwezesha watu wa Ogiek kuenda kuwaeleza wako kwa constituency gani?

**Audience**: Molo

**Com. Salome Muigai:** Molo kuenda kubaliana na ile chama cha huko waseme hiki tuliwapa kura mia nane. Naitakuwa wajibu kuwezesha kuwa na matatu kwa watu wenye kura nyingi kwa chama chenye kura nyingi ni dhaifu, kwa hivyo lazima tukichagua tumpe ngapi? Did see what we are saying. Tunapatiana nafasi ya watu ku-negotiate. Kama ni ndogo, kama wewe ni mingi, yoyote yule mrandi tuwe kutoka wapi. Mkiwa wapi?

**Audience**: Kenya

**Com. Salome Muigai:** Kenya. So that is the part I want to explain kwa nini habari ya composition ya bunge.

Kitu kiingine kimoja na Wakenya walitwambia. Kenya walitwambia ikiwa wapeleka mbunge bunge akienda huko tutamuona tena baada ya miaka tano. Hatutaki tena. Tunataka sisi kuwa na simu yenye tunaweza kumwambia sisi kulikupeleka na sisi tunaweza nini

**Audience**: Kukuiita.

**Com. Salome Muigai:** Kukuita. Kwa hivyo ukisoma hiyo chapter hata hiyo sura utapata mbinu zenye zimewekwa na kisheria za kuwesha kuturudisha naye, mbunge ama diwani wa watu.

Tungepeleka tatu kwenye hiyo sura tunaeleza habari ya kuhitaji more officers and other functionaries. Speaker wa National Assembly ameletwa pia habari ya presiding their National Council na ni mwenya achagua mzungumzaji wa kikao hiki za taifa. Tumezungumshia kila Speaker na deputy wa national Assembly na tumezungumshia kila National Assembly yenyewe, tumezungumshia karani wake, tumezungumshia ile pia wataendeleza mambo yao. The business of the National Assembly. Hiyo mlitueleza mambo mengi vile mngetaka haki gani ama uwezo gani tungetaka kuwa na hawa na tumejaribu kuwafikia na kuwapa.

Tumezungumshia pi ajuu ya mishahara ya watu wa bunge ama ya watu wote. Tumesema kuwa kutakuwa na tume yenye kuwangalia mishahara ya kila mtu anayefanya kazi katika uma. Hata awe ni mbunge, hata uwe ni President, hata yeye ni mwalimu, awe ni daktari, tumesema basi Wakenya walitwambia hawataki kungine kusikia kamwe kuwa mtu ameketi chini akafikilia jambo ndiyo atachukuwa mshahara gani. na hawa ndiyo, ndiyo mwisho. Akisha fikiria ndiyo na kukumbali basi tumefikilia hali ya kuleta madaraka ya kuchagua mambo yao wenyewe.

Tumekubaliana kua Rais bado atakua ndiyo wa mwisho kuweka sahihi kwenye Sheria ya Kenya. Lakini pia tumempa nafasi ya vile atakavyofanya hivi. Akiletewa hilo swala mara ya kwanza amepatiwa muda fulani akiwa swali lazima ajiulize kwa muda fulani, akiwa na tajilizi atauliza what is real code imweleze pia kwa muda fulani akiuliza kwa bunge itakaa muda fulani buda bado zikifilia hizo sheria ile iliye nataka itamrudishia na wakati huo Rais atakua jukumu yake kuwakilisha kukubaliana na hiyo Sheria. In other words tumeweka binu za mawasliano ya Constitution lakini mwishoye tumeweka mpaka kua hatutawasiliana kutokea January mpaka lini mpaka December kwa jambo moja hivyo. Tutaweka kipimo kwa wakati tutaweza fanya hivyo.

Pia tumekubaliza Rais kwenda kwenye Supreme Court na kuuliza washia akiwa na shida yoyote kuhusu Katiba. Tumeweka masiliano katika National Assembly na National Council tumesema kwa sababu fulani fulani National Assembly wenye ni watu tumechagua kwa mambo fulani lazima wasiliane na National Council ambapo ni baraza la taifa. Tumekubalina kikao kimoja kitakua na forum eighteen. Tumekubalina kuwa lugha za bunge zitakua tatu mbeleni zilikuwa mbili. Watawasiliana kwa Kingereza kwa Kiswahili na pia isara. Yaani watu wenye hawasikii na hawazungumzi lazima wapatiwe nafasi yao ya kukubalika kua lugha yao pia inahuzishwa kwenye bunge letu.

Tumekabaliana kwa Standing Orders tumeziwekelea. Tumekubaliana vile miswada tofauti ikatakapelekwa kwenye bunge. Tumekubaliana vile wakati gani utapatiwa kila mswada na kwa muda gani na tumekubaliana kwa kuzikiza Parliament zitakuwa zipi na zitakua na kazi zipi.

Kitengenezo cha tano tumekubalian bunge itakaa kwa muda gani. tumekubaliana ama tumewaziliza bunge itaweza kusimiswa je. Hiyo watu wengi matakwa yao na tumesema radi na basi tumeileta tena kwenu muone kama vile tumepedekeza mnakubaliana nayo. Na tumeleta pia kuwa tunaweza kua na mswada ya kutokua na mswada ya kutokua na "no confidence" inatwaje je? Kutokua na nini?

**Audience**: Imani.

**Com. Salome Muigai:** Na imani na jambo moja ama lingine katika bunge. Na za ziada pia tumeleta habari ya uhuru wa kujadiliana, tumeleta habari na kualinda wanabunge wakati wanapozungumzia hali yetu na tumeleta habari ya vile wananchi wa kawaida watahuzishwa kwenye mujadala fulani fulani ya bunge kua ziwe tu vile nimesampatia mbunge wangu kura yangu azisahau kuwa bado nimeendelea kufikilia na kunihuzisha kwa mambo fulani kabla hajachukua msamwati. Aliye tafadhali wakati mwingi pia kutuuliza kuna maoni gani.

Mwishoye pia tumewekelea madhabu pia Parliamental Service Commission lakini imekuwa na siku moja ama mawili tafadhali ukisoma kwenye utaratibu wa hayo mambo utaona tumependekeza nini.

Halafu tuna mswada wa the Executive chapter 8. Principles and chapter of National Executive tuna the Authority of the Executive. Haya ni mambo yenye imeleta kutoelewana watu wamesema, tumesema, tumemweka Rais asiye na mamlaka. Rais wetu bado ana mamlaka ya kuutunganiza zote tukawa taifa moja. Rais wetu bado ndiyo custodian, custodian ni nani?

**Audience**: …………… (inaudible).

**Com. Salome Muigai:** Mudhamini na mlezi, na nini tena mlizi, mhifadhi hayo yote na mengine mengi ndiyo mwenye kuhifadhi Katiba yetu na ndiyo mwenye kueleza wakati wenye anafikilia kutuita ili tuilinde. Vile ni nilivyosema ni kizungumzia habari ya bunge pia ndiyo mwishoye atakubaliza sheria sivyo. Bado bado ndiye atakubaliza sheria.

Raisi yetu ni Amiri Jeshi Mkuu wa taifa hili. Rais wetu ndiyo mwenye kuhifadhathi uhusiano wetu na mataifa ya wapi? ……….. (inaudible) ndiyo mwenye ataendelea pia kuwachagua watu mbalimbali. Lilo na siasa hapo ni kidogo tu kuwa atawaziliana na watu tofauti kwa mambo fulani atawasiliana na bunge, kwa mambo mengine kama ya machache atawasliana na tume ya kuandikiza wanasheria na watu wengine. Lakini mwishoye jukumu ya uchaguzi wa watu wenye kuchukua mamlaka mbalimbali bado ni la Rais.

Rais wetu atakua ni mtu mwenye atakuja kwenye uchaguzi akiwa na mwenzake rasmi na mwenzake atakua ndiyo Makamu wa Rais. Na huyo mwezake Makamu wa Rais wananchi walituambia wangependa kumchagua moja kwa moja, na atakua ni naibu, msaidizi, muite lolote lile, lakini ni Makam wa Rais wa kweli.

Tumeelezea kazi za Bwana Rais wetu ama Bibi Rais yenye atakua akitekeleza tumeelezea uhusiano kati ya Rais na bunge, tumeelezea habari za nguvu za Rais ni zipi na tumewezeza kukazishwa vipi, tumeelezea habari ya uchaguzi wa Rais, tumeelezea Rais atahitajika kua na qualification. Qualification nini? Kuhitimu vipi ndiyo aweze kuwa Raisi. Tumeelezea maswala ya the validity of Presidential Election, tutaiangalia je, procedure ya uchaguzi wa Rais na mambo mengi mengi. Tumeendelea kusema Rais atakua Rais kwa mihula miwili tu ya miaka tano kila mmoja. Tumeeleza Rais asipokuwako na nani atashikilia mamlaka yake na kukiwa na jambo lenye litafanya tuwe na Rais mwingine tutaendelea na hayo mambo kwa njia gani. Kwanza tumesema Rais akiwa hajiwezi kwa muda wakili wake ni Makamu wa Rais. Wakiwa wote wawili hawako Speaker wa bunge atashikilia mamlaka ya Rais kabla hatujafanya uchaguzi. Haya ndiyo yenye mafpya yenye tumeongeza. Tafadhali some ile sura ndicho kipengele cha pili habari ya Executive kina mengi ya kuwasiliana.

Tumesema kuwa Prime Minister atachaguliwa na bunge kutoka kwa chama kilicho na waakilishi wengi zaidi kwenye Bunge. Yeye atachagua Cabinet. Cabinet inaitwa nini?

**Audience**: Baraza la mawazili.

**Com. Salome Muigai:** Baraza la mawaziri. Pengine nikinywa maji kidogo nitakumbuka Kiswali lingine. Atachagua baraza la mawazili wakuhusiana na Bunge na pia Rais ndiye atakayo chagua mwishoni ni Rais atakua na mamlaka ya kusema huyu ndiye Waziri Mkuu.

Tumeeleza pia juu ya kazi ya Waziri Mkuu, atakua na makamu wawili. Tumeeleza kazi yao wawili, tumeelezea pia baraza la mawiziri, pia tumesema kuwa baraza la mawazili Nitachaguliwa kutoka kwa wataalaam. Hayo ni mambo yenye kila Mkenya zaidi ya Wakenya 90 percent walitueleza kuwa wanataka mtu mwenye kusimamia elimu akuwe nini? Akuwe ni msomi. Wanataka mwenye atakayekuwa akisimamia afya yetu akuwe daktari. Wanataka mtu atakayesimamia majeshi yetu awe ni askari. Na mwenye atasimamia sheria yetu awe ni mwanasheria. Hizi tuliambiwa kutoka kwa wananchi. Swali moja na lenye tumeuliszwa muda kwa muda ni kuwa kwa nini mumesema kwa nini mawaziri hawatoki kwenye Bunge?

Wananchi pia walitueleza mambo mawili. Wametuambia jambo moja mbunge wetu akiwa waziri hatuna mbunge tena. Ni yenye yuko pahali fulani. Nani ana dhaifu leo na kesho na kesho kutwa sisi wenyewe hatufanyi nini? Hatumuoni, utaona mbunge siku nne Rais atakuja kufanya nini? Kututembelea. Kwa hivyo wambunge tumewaachiza kazi ya kua wambunge na kuwa mawaziri.

Mbunge akiwa waziri, kukiwa kuna mbunge mwenye Prime Minister angetaka kutoa kwenye bunge ni lazima mbunge ajiuzulu. Pia siku moja tuliambiwa na wananchi ni kuwa tunataka mtu mmoja akue na kazi ngapi?

**Audience**: Kazi moja.

**Com. Salome Muigai:** Akuwe na kazi moja. Kwa hivyo ukiwa mbunge na ukuwe waziri una kazi ngapi?

**Audience**: Mbili.

**Com. Salome Muigai:** Una kazi mbili na ukipika kumili moja inafanya nini?

**Audience**: Huungua.

**Com. Salome Muigai:** Moja huungua. Kwa hivyo tunataka wakati Kenya mpya, pahali kila ya kuna mtu atakuwa na jukumu moja, na tumuulize baada ya muda fulani umetufanyia nini kwa kazi moja tuliokupa? Hii tumetoa kwa wananchi.

Jambo lingine lenye tuliambiwa na wananchi ni kuwa wakati wabunge wako Bunge na wanajuwa kua wanaweza kua mawaziri mara nyingi wanaogopa kuzungumza kupinga mambo. Kwani wanangoja kuchaguchaguliwa nini? Mawaziri, na ukipinga mara nyingi nyingi hautapata nini?

**Audience**: Uwaziri.

**Com. Salome Muigai:** Uwaziri. Kwa hivyo tunataka kutenganidha uwaziri na ubunge. Pia hiyo ni kutenganisha madaraka. That is part of demokrasia. Demokrasia inasema mamlaka ya Serikali ni lazima yatengane kwa kiwango kinacho wezekana. Kwa hivyo mtu akiwa ni mbunge asiwe pia ni part ya executive ya Serikali. Kwani Serikali ni Rais na Prime Minister na Cabinet. Hicho kiwe kiwango kimoja.

Kiwango kile kingine kiwe ni mbunge mwenye anatengeneza sheria, na kile kingine kiwe ni mahakama na ma-judge. Kwa hivyo pia ukiweka hii kwa kujaribu kutenganisha mamlaka ya nini?

**Audience**: Serikali.

**Com. Salome Muigai:** Tukielewa tutajua kama ni vizuri ama ni vibaya. Lakini tusipoelewa kwa sababu gani tumekuja itakuwa shida kufikiria hali gani ile tutaweza kufikiria.

Tumefikiria pia habari ya Permanent Secretaries na kuwaweka kwenye Katiba kwa ajili walikuwa wanatakiwa wawe katibu wa kufanya nini? Kama ni Secretary ni katibu wa kufanya nini?

**Audience**: Kuhudumu.

**Com. Salome Muigai:** Kuhudumu lakini siku hizi wanahudumu?

**Audience**: Hapana.

**Com. Salome Muigai:** Tunataka kuwafudisha ndiyo tunawawezesha pia kwenye Katiba. Pia tumeleta habari ya kiapo chenye kitachukuliwa na wale watu wenye watapatiwa wadhifa tofauti.

Chapter Nine: hii sijui nikizungumzia bado niko huru lakini basi nitazungumzia tu. Hii ni Judiciary and Legal System – yaani mahakama na judge. Tumeelekeza nguvu, tumezungumzia juu ya nguvu ya mahakama. Tumeweka korti tofauti kwenye mahakama. We have introduced tumeleta korti mpya yenye Supreme Court inaitwa korti gani? Korti kuu? Nafikiri ni kuu.

Supreme Court angalia kwenye mswada. Supreme Court ndiyo yenye itakuwa na jukumu na mbili. Mmoja ni kuangalia habari ya Katiba. Ukiwa na swali lolote juu ya Katiba utaenda moja kwa moja kwa korti kuu.

Ya pili itakuwa ndiyo mwisho wa rufani, ukisha enda kwa korti ya magistrate, ukaenda kwa High Court, ukaenda kwa Appeal Court mwishowe utafika wapi? Supreme Court, na hiyo itakua ndiyo korti ya mwisho. What is the …………. (inaudible)? Mahakama ya juu kabisa. Hiyo tulikuwa tumeshatatua sisi wenyewe sivyo.

Tumezungumzia hizi korti tofauti zitakua na majukumu gani? Zitakuwa na kazi gani, moja kwa moja tumeangalia hizo korti zote, tumezungumzia vile judge watakapokua – judge anaitwa nani? Hakimu- vile hakimu atakavyochaguliwa. Tumezungumzia habari ya kulinda kazi ya hakimu ili aweze kutekeleza jukumu lake. Tumefikiria hakimu wakifanya nini watatolewaje kwenye mamlaka hayo. Tumeeleza korti ya Kadhi, tukaipa levels, viwapo mbalimbali za zamani ilikuwa moja peke yake. Kwa hivyo wakati huu kuna viwango tofauti.

Pia tumeangalia vile Kadhi atakapochaguliwa tukasema lazima Waislamu wahusishwe. Na kuwa Kadhi atakuwa yeye ni mwenye korti peke yake hatakuwa msimamizi wa dini. Kazi yake itakuwa uhakimu hata kwa kuhitimu kwake tumesema tumeandika kuwa ni lazima uwe amehitimu sheria na mambo ya Kiislaam.

Swali lenye tumeulizwa kila mahali lilikuwa kwa nini tuna korti ya Waislaam hatuna Korti na hatuna korti ya Wakristo? Hii ni kuwa makubaliano ya zamani sana nafikiri sijui kama ni 1926 wakati unajua Coastal Strip kulikua maili kumi ilikuwa bado ziko kwenye mamlaka iko kwenye mamlaka ya Sultan. Wasipokubaliana na Kenya kuwa itachukuliwa na kuwa ni ardhi moja ya Kenya. Jambo moja lenye pia lilikubaliwa ni kuwa Waislaam watakubalishwa kwa minajili ya sheria ya kibinafsi kufuata dini yao. Na kina mama Waislaam wanatuambia kama wakati akina mama bado wanapigani urithi, ilikuwa Waisalam wanakubalishwa zamani sana kuwa na urithi chini ya mamlaka ya Kislaam. Pia walitwaambia kuwa hii habari ni kuwa ya

kwenda kusikiza watu tofauti Kenya imekuwa masomo ya kipekee sana kwenye sisi wenye tume. Walitwambia kuwa ukitoa kwa dini ya Kiislaam ukitoa mali ya kuoa, mali ya kuoa inaitwa je?

**Audience**: Dowry/mahari

**Com. Salome Muigai:** Mahari unampatia bibi mwenyewe sio baba yake wala sio ukoo. Sisi akina mama tunafikiria pengine huenda tukaanza kuwa Waislaam sisi zote. … (laughter). Kwa hivyo tumeengalia mahakama mbalimbali pia tumewekea mamlaka zaidi Judicial Service Commission. Tume ya kuajiri majaji ili iwe na haki kubwa za kusema huyu hawezi kuamliwa hakim kwani kuna kesi zenye bado watu wamemshitaki kufanya hivi. Alipokuwa advocate wa Kitale alifanya hivi na vile na vile kwa hivyo tutachunguza watu, kutakuwa na tume tofauti za kuchunguza hakimu kabla hajaletwa kuwa hakimu.

Tumesema kuwa mishahara ya hakimu itaangaliwa pamoja na mishahara ya wafanyikazi wote wa uma, ili tuone kuwa hakuna mtu mwenye kupata shilingi elfu mia moja kila mwezi na mwingine mwenye kupata shilingi elfu tano, na wakienda kununua unga wananunua kwenye duka moja.

Halafu jambo lingine na lile tumefanya ni kuelekeza habari ya sheria, ni kuwa tumetenganisha afisi ya Attorney General, anaitwa nani?

**Audience**: Mkuu wa Sheria.

**Com. Salome Muigai:** Mkuu wa Sheria, tunaambiwa tumuite mwanasheria mkuu kwani hakuna mwenye ni mkuu wa sheria. Kusema Mkuu wa sheria, ni kusema ni kuu kuliko nini?

**Audience**: Sheria.

**Com. Salome Muigai:** Sheria. Lakini jambo moja lenye tumefanya ni kutenganisha hiyo afisi yake ikafanywa kuwa na afisi mbili. Moja anakuwa ni wakili wa serikali. Ni advisor – legal advisor wa Serikali. Mwingine ni mwenye kushitaki. Tukasema wakati mwingine hizi afisi mbili zina ………..

**Audience**: Tetanisha.

**Com. Salome Muigai:** Tetanisha. Wakati mwingine mtu anataka kuipeleka hiyo Serikali kortini. Na huyu mwenye lazima akupatiye kipawa cha kustaki pia ndiye ..

**Audience**: Mkuu wa Sheria.

**Com. Salome Muigai:** Kwa hivyo sasa tumeifanya kuwa afisi mbili moja ni ya Attorney General na huyo ni advisor to the Government - Legal Advisor kwa Serikali. Na hiyo nyingine ni ya public – the Head of Public Prosecution. Huyo ndiye mwenye shitaka zote, na itakuwa afisi mbili tofauti.

Pia tumeleta afisi mpya ya Public Defender. Mimi nikishtakiwa, ama nikiwa nimetatizwa na hii Serikali, nitasikizwa na Serikali yangu, naenda kwa nani? Tumeweka Public Defender yeye atasikia malalamiko yako, atawasiliana na wizara yenye kutatiza na wasipokubaliana atakuwa na nafasi ya kuwasilisha kesi yako kortini. (clapping)

Kipengele la tatu katika hiyo nafasi – hiyo nyingine endeni musome. Tukubaliane this is just an introduction. The third part in the Profession of Law. Pia hii ni utalaam wa sheria tumewekea the proposals zenye mutaangalia muone kama mnakubaliana nazo. Chapter ten: hapa ndiyo pahali mkodo wa mambo ulipo. The devolution of powers. Watu wengi walitueleza kuwa Serikali ya Nairobi, iko mbali sana na sisi. Hata kwenda kuifikia yenyewe wakati mwingine tunauza shamba na ngombe ndiyo upate nauli pa kwenda Nairobi na hata ukienda huko pahali ya kulala panakua shida, chakula yakua shida. Tungetaka Serikali ilio karibu na sisi. Na sasa tumeelezea kwa nini tunataka kuleta uongozi karibu na watu. Tumekuwa na head of principles. Na tumesema organizations, tumeweka organizations za hiyo devolution ni zipi. Tumeleta principles/maoni yetu kwenye hiyo devolution na tumeleta levels tulisema ni viwango? Viwango tofauti vya Serikali. Tumeleta Serikali katika location. Yaani location itakuwa na Serikali yake. Tutaendelea kuzunguza mmoja kwa vingine hii Serikali tungeta iundwe namna gani.

Tumesema pia tunataka mambo mengi sana ya utawala ije kwenye Wilaya. Mambo ya Transzoia yaje Kitale hapa. Tuwe na Serikali hapa Kitale yenye kuangalia habari ya afya yetu, yenye kuangalia barabara zetu, yenye kuangalia elimu yetu na yenye kuangalia mambo yetu yenye nia pekee katika Kitale. Kwa mfano mambo ya mahindi iko karibu sana na nyoyo watu wa Kitale sivyo. Isichanganywe na watu waweza kuzikishwa wenye wako na gari ama ichanganywe na watu wakati wake wenye wako na wanataka tupate kitu ndiyo na ichanganywe na mambo ya Kisumu wenye wako na mali. Sisi wenyewe tupatiwe nafasi yetu ya kufikilia mambo yetu Tumesema pia kwenye ukoa kutakuwa na Serikali lakini Serikali dogo katika – kazi yake ni coordination. Ni kuangalia habari ya Tranzoia na habari ya mila yetu tuko hapa ya Turkana, ya Marakwet, Keiyo, Uasin Gishu, Nashu, yaani kazi yake ni kuangalia kuna jambo gani linafanyika hapa, kiru gani watu wa Uasin Gishu na Tranzoia wangetaka kuhusiana. Basi itakua kazi ya Serikali yenye itakuwa kwenye mkoa ya kuhusiza pahali yenye inatakiwa. Bona sio hivyo watale watu wa Tranzoia waendelee na mambo yao.

Pia tutakuwa na Serikali ya National ya Taifa nzima. Hiyo yenye itaweza kusema kunayo watu wa Tranzoia wana ugali ya kutosha mali nyingi wanaweza kaa wakati hakuna sukuma wiki. Kwa hivi inatakiwa watu wa Kisumu tufanye vipango vile watawaletea omena kidogo. Kwa hivyo kutakua naye coordination hata national level. Lakini mambo ya muhimu na mambo ya kila siku kwa kila Wilaya itafanyika kwenye Wilaya. Pesa za lenye itatoka kwa Serikali ya taifa ikija kutoka huko itakuja kwenye Wilaya. So the gap of implementation of the policy will be at which level? At the District Level. Hiyo pia itahitaji mtu

asome kwa kinaganaga ndiyo aweze kuelewa itafanyika vipi. Na pia kutakuwa na sheria yenye itatungwa kwenye hiyo Wilaya. Kwani ukitaka kutunga sheria za mahindi na ni za muhimu kwa Tranzoia zaidi ya Kajiado, lazima tuwakubalize watu wa Tranzoia kutunga zenye zinahusiana na mambo yao. So there will be different levels of regislation of laws. Na Provincial pia itakuwa kazi yao za hamonization na pia at national level will do a national hamonization. Hizi vitengele vinatakiwa kusomwa kwa ustadi kubwa kabla hatujakubaliana na ndiyo tumewandikia hii report ili msome na muelewe na zungumshe moja kwa mwingine ndiyo kabla hatujafika kwenye kikao cha kitaifa tuwe sisi wenyewe tumekubaliana mambo ambao tunaweza kukubaliana kwa kikao hiki.

Sura ya kumi na moja ni sura pia yenye utu mkubwa kwa watu wa Kenya. Land and Property. Habari ya mashamba. Tumekubaliana kuwa lazima tuwe na post moja ndiyo ya kuelezana habari ya mashamba katika hii nchi. Na moja tumekubalina ni kuwa ni ya watu wa Kenya. Ile yenye hao watu wanaweza kupatia kikundi fulani kwa sababu fulani. Lakini shamba ni ya hasani ni ya watu wa Kenya. Tumekubaliana kuwa tutakua na classification, tutakua tofauti ya mashamba. Kuna yale mashamba itakuwa ya watu binafsi, kuna ile shamba yaweza kuwa ya jamii family, kuna shamba yenye itakua ya jamaa, a community na tutarudisa nguvu kwenye jamii, jamaa. We are going to give them, we giving the community back the powers to be able to look after its lands. So we have gone back to the communal rights tunayo. Haki ya jamaa ya kuangalia mashamba yao.

Tumekubaliana kuwa Kenya of lands inahitajika kuangaliwa kuwa hakuna mgeni mwenye atakubalishwa kununua shamba katika freehold. Mgeni yeyote asiye Mkenya ni lazima apatiwe shamba kwenye lease. Tungetaka kusikia matakwa yenu juu ya freehold itakuwa miaka mingapi. Watu wengine wamesema miaka tisaini na tisa ni nyingi sana. Tuende kwa miaka hamsini. Lakini nitangaalia na unafikilia gani yenye itakuwa muhimu na mtatueleza.
Tumefifia tungetaka watu kurudishiwa mamlaka ya kulinda mashamba yao na kulinda ardhi yao. Yangu ni kuwa tunasema hii ni ardhi yetu ni ardhi zitu sisi kama wananchi tumekaa hapa tuwe na haki ya kulinda hiyo vitu yetu. Na kila mtu anaweza kuenda kortini wakati huu kusema mimi nimekuja kwa ajiri matumishi baya ya ardhi ya pahali ninakaa. Mbeleni tukienda kortini unaambiwa huna locus standi sijui wana sheria waita nini. Kila mtu sasa ana haki ya kuenda kwenye korti na kusema hii ardhi ni yetu inatumika vibaya hata mimi ninavyotumiwa hatutaweza kuipatia vizazi vijao. Kila mtu sasa ana hiyo haki.

Na hiyo inafuatana sasa ni sura inafuatia ya mazingara. Kuwa lazima mazingara yetu ilindwe kwa vizazi vilivyo sasa na vizazi vijao tumeweka tume ya kulinda mazingara yenye yatawazilishwa kila pahali na pia tumejipatia nguvu na haki za kutekeleza kazi yake na tumefikiria kuwa kutoka hiyo Serikali ya kijiji mpaka Serikali ya taifa ni lazima uwe na sheria za kulinda mazingara. Kutakuwa na sheria zenye zitahitajika kwenye masinani, kutakuwa na sheria zenye zitahitajika kwenye mkowa na pia kutakuwa zenye zitahitajika katika taifa zima.

Sura ya kumi na tatu ni juu ya Public Finance and Revenue Management. Yaani habari ya pesa za umma na nyinyi tena. Sasa hamnisadii kwa Kiswahili mumeniachia. Mumechoka?

**Audience**: Hapana.

**Com. Salome Muigai:** Sasa tulianza na nyinyi, mimi ikaanza, mumechoka mbele yangu na nyinyi ni wengi? Public Finance and Revenue Management ni nini?

**Audience**: Pesa ya umma

**Com. Salome Muigai:** Pesa ya umma na nini?

**Audience**: Uzimamizi wa usuru.

**Com. Salome Muigai:** Usimamizi wa ushuru. Good. Sasa hapo pia tumeeleza lengo zetu pia vile tunataka hii pesa tunaka zimamiwe. Habari ya ushuru, tumesema jambo la kwanza kuwa hakuna mtu yeyote atayesimamiwa asilipe ushuru. Na akikubalishwa asilipe, baada ya miezi tatu lazima msimamizi wa ushuru ambeye aliempa hizo ki-power za kukosa kulipa, aende kwenye bunge aeleze sababu gani zilifanya huyo mtu aziitishwe ushuru. Whether he is an income tax, kama ni position, chochote kile kila mtu ni lazima alipe akisimamishwa asilipe lazima bunge lielezwe ni sababu gani.

Hiyo ni jambo kubwa lenye tume-introduce. Jambo lile lingine la muhimu lenye tume-introduce ni kuwa tungetaka kuona uhusiano kati ya ushuru na sub-provision. Tukilipa ushuru tutapata nini kutoka kwa huu ushuru. Akautambilizi, tunalipizwa kila mtu na sasa anasikia kuwa tunalipa kwa kila litre kwa kila litre ya mafuta sijui tunalipa ushuru wa pesa ngapi. Tunataka kujua zinafanya nini. That is another function.

Pia tumesema kuwa wakati Auditor General anaposimami hesabu ni kama kufunga boma kama ngombe tayari amesafanya nini? Amesha toka. Sasa tunataka hizo viti ziwe viti mbili. Moja ni ni mtu akisimamia ngombe izitoke sana kwana. Hata ukisema hii itoke dakika mbili iende ikamuliwe, hii ni ya kulima …. tunataka kuwe mtu hapo mwenye kuchunga. Halafu pia tuta-afford Auditor General wa kusema hata badala ya kuchunga hivi matumizi yalikuwa hivi. So there being ………… (inaudible) we are trying to monitor and then ……… (inaudible). Hiyo kiti zimeondolewa moja kwa nyingine vikawa afisi mbili. Tumewapatia hawa watu wawili hudumu wakati wao, protection Kenya ndiyo pia waweze kufanya kazi yao.

Pia tumeweka tume ya Economic and Social Council. Hii ndiyo tume yenye itangalia. Tunawezaje kwa muda fulani watoto tisa nne kwa mia walikuwa wanaenda shule na wakati huu watoto sabini kwa mia ndiyo wanafanya nini? Wanaenda shule. Na wakati huu wakati wa waalimu hawajalipwa watoto wangapi wanaenda shule? Acha wao hawaendi hao sabini. So this Economic tume ya uchumi na social nini nini. Jamii la uchumi ndiye lenye itakuwa ikipiga dharubini mambo isifike mpaka hapo ikaharibika vipi, vipi ilivyo kabla hatujafanya jambo juu yake. Itakuwa na jukumu ya kuyangalia kuona hazifiki hapa tena.

Sasa ndiyo tumemalizana na shura ya kumi na tatu. Tuko kwa shura ya kumi na nne. Public Service. Tumeelezana kuwa tuna haja ya kuwa na public service iliyo na nguvu zaidi. Tumeeleza wanatume wa Public Service watachaguliwa na nani na watachaguliwa kifipi. Na watakuwa mswada gani na watasimamiwa vipi ili weweze kufanya kazi yao vilivyo. Tumekubaliana kuwa watarudishiwa kazi yao ya uwajirizi. Kuwa hakuna organ nyingine ya Serikali yenye itakuwa na jukumu ya kuajiri. Kama tunataka Permanent Secretary tutoa majina kwa Public Service Commission, watutueleza kwa sababu gani fulani ndio mtu anaweza kufanya hii kazi itakubaliwa hata kwenye bunge na imekuwa mwisho kama ni Rais ili tuwapate. Kwa hivyo Public Service Commission.

Tumeleta pia tume ingine ya Kenya Police Service. Kila pahali yenye tuliambiwa kila mtu alilamika kuwa Police wakija hapa kutafuta wafanyi kazi watoto wetu wanakimbia wama hema wanafanya nini na hatuoni wakiajilia. Kwa hivyo hii Public Service Commission and the Public Service tutawauliza kuwa kwenye population tuna wabukusu. Kwa nini hakuna moja kwenye polisi. Munawatoa wapi? Kwenye population tuna Ogiek watano, hatuna moja kwa polisi, hatuna moja kwa pahali fulani, hawa watu wengine mnawatoa wapi? There would be somebody accountable na watapeana habari zao zenye zitawazilishwa kwenye bunge ndiyo wengine tusikie kuwa watu wa Kenya wanazuru kifiki kwa ujenzi wa taifa lao.

Tumefifia pia habari ya magereza yetu. Tulipata mambo mengi kuhusu haki za kibinadamu kwenye zinawezaje kuangaliwa na kuwangaliwa kwa dhati tulizungumsha na wakuu wa mangereza na pia tulizungumza na wafungwa. Na part ya tatu kwenye hiyo sura ya – kitengenezo za tatu katika shule ya kumi na nne kimeongelea habari ya mambo ya urekebizaji wa tabia. Collection of Services.

Sura ya kumi na tano imeangalia habari ya Defence and National Security. Kuna mambo mengi sasa yenye tuliambiwa na wananchi kuhusu usalama wa nchi na wakakubaliana kuna mambo nyingi yenye tulikuwa tunataka tuangalia. Kwa hii Katiba mpya tumetoa mswada wa kuazinza tume ya usalama wa nchi ama kikao na usalama wa nchi. Tukitaka ofichwa National Security Council. Watu watakuwa wanaingia. Kwa hivyo bado Rais ana mamlaka ya kuangalia watu wake.

Nitangalia habari ya Defence Forces na itangalia kina nani wanafanywa kuwa Commanding Officers. Itakubaliana na hii council hao wenye kuchaguliwa kuwa commanding ndiyo wenye wanatakiwa kukuwa kwenye hizo vyoo.

Kwenye sura ya kumi na tisa tuna Leadership and Integrity. Tutakuwa na kamati ya kuangalia watu wenye kutaka kusimama kwenye viti vya leadership. Vya uongozi. Watakuwa wakiwakiliza mitihani yao wenyewe. So that it is not enough that I am graduate and I want to be President. They to check on my conduct, who I am I, what is my discipline, nilipokuwa kijana wa university nilifanya nini? Nilikunywa bhangi. In other words accountability kwa Wakenya ndiyo wakati wenye mtu anasimama kuwa anataka kuwa kiongozi ajuwe kuwa maisha yake ya kibinafsi ametupatia sisi. Kwa nini amekuwa kiongozi wetu?

Chapter seventeen – Constitutional Commissions. Kumekuwa na tume zenye zinaingilishwa Kikatiba, tumezungumzia kwa

jumla maoni yetu juu ya kuwazishwa kwa hizi tume, tumezungumshia lengo ya hizi tume na uhuru wake wa kufanyia kazi yake zitawekwa pamoja vipi. Wanatume wenye watachaguliwa wanachaguliwa kifipi. Wataondolewa vipi, kunapo mlango wa kuingia lazima kuwe na wa nini?

**Audience**: Wa kutoka.

**Com. Salome Muigai:** Wa kutoka. Na ndiyo na nini? Wananchi wanataka kuweza kujua kwa hivyo kila mwaka na zingine zaidi mara mbili kwa mwaka au mara tatu kulingana tume wenyewe itawazilisha report yake kwenye bunge kuwaeleza vipi wanafanya kazi yao.

Tutakuwa na tume ya Katiba. Hii tume itakiwa na kikao kimoja tu cha miaka tano. Kazi ni kuhakisha kuwa hii Katiba inatekeleshwa. Bunge imetunga sheria zinazokubaliana na hii Katiba na pia imerundia zile sheria zenye haziambatani na nini? Na Katiba. Kwa hivyo hiyo itakuwa kikao kimoja tu cha miaka tano baada ya miaka tano, miaka miwili tutaiuliza umefanya kazi gani, tukisikia bado inafanya kazi nzuri tutaiambia iendelee, tukisikia haijafanya chochote bado ya mwaka tutaambiwa jamani kwa herini ya kufanya nini?

**Audience**: Ya kuonana.

**Com. Salome Muigai:** Kwa herini ya kuonana. Tuchaguwe watu wengine, lakini zaidi tungetaka mwanzoni, mwanzoni kuchagua watu wenye watafikilia na wataweka kwa dhamana hii kazi kubwa, jukumu kubwa na waweze kuiyeleza. Lakini hatutaki kuimba muhula mwingine baada ya miaka tano. Hatutaki iwe kazi ya kila siku. Kuna pia tume ya haki za binadamu na Administration of Justice kuwadimisha uhaki na hiyo itakuwa ikiangalia haki zako na vile zinaendelea na pahali gani inakiukwa. Moja wa hao watu wenye watakuwa pia ana jukumu ya kuwangalia haki za watot, moja atakuwa na jukumu ya kuwangakia haki za walemavu na huyo atakuwa pia mulemavu. Watu wanasema mtu mwenye kuvaa viatu ndiye anajua nini?

**Audience**: Kinauma pahali gani.

**Com. Salome Muigai:** Kinauma pahali gani. Ukijaribu kumweleza mtu mwingine akwambia a ningali kwenye kwenye buba na pale kwenye kidole kime……….. ama ni pande gani. Lakini mwenye kuumwa angeweza kukuza hata kama kuna giza ataguza wapi?

**Audience**: Pahali penyewe.

**Com. Salome Muigai:** Kwa hivyo tunataka watu wenye wataweza kuelewa shida za watu walio na ulemavu.
Tutakuwa pia na Ethics and Integrity Commission. Hiyo ndio yenye itachunguza mienedo na tabia ya viongozi watu wenye

kutaka uongozi na usoni.

Tutakuwa pia na hiyo tume nilizungumshia kifupi mbeleni yenye itakuwa ni Salary and Remuneration, mishahara na malipo yenye saa jaribu sana kufanya kuwa kila Mkenya anapata mshahara mwenye unawezesha kuishi maisha yenye nini? Yenye diginity. Yenye nini?

**Audience**: yenye ustaraaf, yenye heshima, ya kusahihi.

**Com. Salome Muigai:** Yenye heshima ya kusahihi, good. Pia Teachers Service Commission wametuomba mara nyingi sana tuweke tume yao kwenya Katiba kwani wamekuwa na shida zenye kila mtu anaelewa. Hizo ndiyo tume, lakini pia takuwa na Constitutional Offices kama zile tulivyosema afisi ya mwana sheria mkuu, ofisi ya Auditor General, hiyo ni afisi zenye itakuwa imesimamiwa kwenye Katiba.

Katika sura kumi nane tuna Amendment of the Constitution. Inaeleza njia gani zenye hii Katiba mpya inaweza kugeuzwa. Kuna nafasi ya wananchi kuhusishwa kwenye mambo fulani fulani. Kuna pahali tumesema hii haiwezi kubadilishwa kabla wananchi hawajaombwa kusema wangetaka lipi. Mtasoma mtaona sheria zipi zimebadishwa mpaka tuzungumzie moja kwa mwingine.

Halafu chapter nineteen ni interpretation. Inaleta kuwa inaleta distination. Tukisema wananchi wa Kenya tuna mara gani? tukisema hiki tuna maana ili tuweze kuelewana pamoja.

Chapter twenty ina mji mkubwa. Inaleta traditional elements. Kuna siku zingine imekuwa tuko na Katiba yenye bado tuko nayo na ina mambo mengi yenye imetufanyia. Imetuleta miaka arubaini karibu na sio kitu ya kubadilizwa. Kwa hivyo chapter twenty , sura ya ishirini inaleta utaratibu wa madiliko. Yaani kama hatujaleta hivi kitu gani itanyika. Kitu gani kwa muda fulani itafanyika ili tuweze kubadiliza Katiba yetu.
Nyingine ni zenye tunaita Amnesty kuna map, kuna code of regulations, kuna mambo mengine yenye kufuatana na hili Katiba mpya. Na kwa hayo maneno mengi sana mabibi na mabwana hiyo ndiyo Katiba mpya. Asante.

Sasa ningependa kuomba wenye maswali na ningetaka sijui kumuomba Bwana Satia angekuja hapa akanisikia ushukani ya akaanza kuwa chair na mimi nizikiliza maswali. Ni shida kuwa chair ndiyo nasikiliza maswali. Bwana Satia.

**Bwana Satia**: Samahani kwanza sasa tutoe maelezo sisi ambayo tungesema kazi ya ……. (inaudible) kubadiliza Katiba. Tutafanya hii, tutachukua maswali karibu kumi hivi kwanza. Commissioner atayadika chini ndipo baadaye ataanza kuyajibu moja baada ya ingine. Halafu akishamaliza hivyo tutachukuwa tena maswali mengine na wengine, na wengine. Hivi tunaposikia mwisho kila mtu awe amefika kwamba yale maswali yake yametauhivyo.

Ya pili tungalipenda kwamba labda unapotoka kutoa kama ni hoja au unataka kuliza swali, tafadhali kwa sababu ya kuweko na watu wengi tungalipenda sana ikiwa utaelezea kwa ufupi zaidi. Ukiwa na maelezo mengi kabla ya kuuliza swali labda watu wengine wanakasiriza kama imekuwa mbeleni na tungalipenda kila mtu afurahiye shughuli yetu. Kwa hivyo hebu Commissioner atueleze kidogo halafu mwanze kupata nafasi ya kutoa hoja.

**Com. Salome Muigai:** Pengine tukianza kwa nafasi ya maswali ningetaka kujibu mengine haijaulishwa ndiyo tukitoka hapa tunaenda wapi? Sasa kwa ile sheria yenyewe imetutunga sisi kama wanatume inasema nyinyi mulikuwa na siku thelathini za kujadiliana juu ya hii Katiba. Lakini hiyo siku thelathini kutoka siku ile tulipoitoa ilikuwa tarehe ngapi? Ishirini na saba? Ishirini na nane? Basi wakati huo sasa kufikia leo muna siku ngapi bado? Tumetumia ngapi? Sisi niliwambia sisi ni waalimu? Mimi nafanya kazi ninapata mshahara ningechukua nikifikilia wakati tulikuwa ni akina waalimu na wafanyi kazi ndiyo tunafanya homework. Twelve days kwa hivyo tumetumia twelve days. Zimembaki ngapi?
**Audience**: Sixteen

**Com. Salome Muigai:** Zinakuwa tatu. Sixteen kuongeza twelve. Kwa hivyo bado tuna siku kumi na nane. Kulingana na sheria ilioko baada ya siku hizo kumi nane nimeambiwa tuanze kikao cha Kitaifa chenye mtakuja na kuzungumzia juu ya hii Katiba. hicho kikao cha Taifa kitakuwa na wambunge wote na mia mbili kumi na wawili. Pia kutakuwa na wajumbe watatu kutoka kwa kila Wilaya. Kwa hivyo tayari pengine nafikili mnajuwa wajumbe wenu. Kwani kulifanyika mkutano na wakachaguliwa. Ni jukumu yangu kumjua mjumbe wako ni nani?

Haya pia kwa wao tutaleta 20% ya watu kutoka kwa civil society. Kwa hivyo watu wa dini, akina mama, walemavu, watalaam, professional pia wakileta watu wengine kikundi chenyengine cha watu. Kwa hivyo kwani wewe ndiyo utakosa kuja hapa kila mmoja wetu hakikisha umejuwa kwako hapa twajua kunatoka akina nani. Na uhakikishe kuwa kati ya sasa na tarehe kumi na nane nyinyi mumeungana kama kikundi ama mtu binafsi na mumewakilisha wajumbe wetu kitu gani mnataka kutoka hapa? Ili wasije kuzungumzia mambo yao wenyewe. Walete sauti za watu kutoka hapa.

Kwenye hiyo kikao tungetaka kufikilia kuwa watu wakuwa Najero Consistance. Vile niliwalifu kwenye tume, tulikatalia mbali sababu ya kupiga kura, tukasema hatutaki kupiga kura. Tunataka kuzungumza na tuzungumshe tena lakini kati tunzungumze tena tena tutafanya nini? Tutazungumza mpaka wakati tutakubaliana. Tutapata concensus. Concensus sio kusema kila mtu jambo lake limekuja vile lilivyo, ni kusema kama tulisema kama tungetaka kuvaa nguo ndefu, mwingine amevaa na mwingine alitaka tufaaye suruari ya kinyaza. Pengine tukikubaliana tutavaa nguo za katikati. Pengine hatutapata hizo nguo za kinyatha, hatutapa urefu wa nguo yangu ile nimevaa leo lakini huenda tutakubaliana pahali katikati. Kwa hivyo hiyo ni wakati wa kuzungumza ukiwa uko tayari kuwazikisha wazako na uko tayari kubadili nia.

Kukiwa kuna msimamo mwenye huwezi fayanya katakata hata usijaribu. Wakati wa Katiba sio wakati wa msimamo usio

badilika. Wakati wa Katiba ni kufikilia mimi pia nilikuwa zijafikilia namna hiyo. Kumbe ikija hiyo inawezeka.. inawezekana. Kwa hivyo nyote ikiwa itaendelea vile sisi tunaupangiliwa tutakuwa na mkutano huu pengine kutokea ishirini na nane.

Jambo lingine lenya ningetaka kujibu ni kuwa sasa hatuna mamlaka yeyote ya kumweleza Rais ya nchi hii anaweza kuvuja bunge siku gani. Kwa hivyo isiinue mkono ukangoja dakika ishirini na tano mkono wako upate nafasi halafu uniulize, je Raisi nyinyi mtafanya nini? Sisi ni wanatume mkitupatia kikomo fulani na ndiyo tunafanya nini, tunaedeleza sisi naye wena Kenya tumpempatia jukumu fulani naye anafanya naye anaendeleza lake.

Kitu moja ningetaka kusema ni kwamba sisi kama watume kazi inaisha January 3. Kwa hivyo chochote tukachofanyika kabla ya hayo ikiwa bunge itafikilia lingine, sisi kufikilia tarehe tatu January kama tume tumefujika. Kwa hivyo maswali ningetaka kujibu moja kwa moja ndiyo msiniulize. Asante. Sasa munaweza kuniuliza yale mengine.

**Bwana Satia**: Asante Commissioner, maelezo mengine tunapata haza tumaliza na maelezo. Ningelitaka kwamba unatuuliza swali ukimaliza kuliza swali. ……… (inaudible) wameketi pale katika ile meza iko hapo mbele ningalipenda habari kuhusu jina lako, anwani yajo na kama unavyo wakilisha mwenyewe au unawakiliza kikundi ili tuwe na record ya kuonyesha kwamba tlikuwa pale ni kwa sababu majina. Watu wangapi walichukulia vitabu baada ya hapo wangapi wameuliza maswali ile tuwe na kuhakisha kwamba mambo haya yameulishwa na Wakenya. Isemwe baadaye kwamba haya ni mambo ambaye ilifikiliwa na mtu fulani fulani.

Na pia unapochukuwa nafasi ya kuliza swali uwaze kwa kujielezea wewe ni nani. Utaje jina lako. Micro-phone iko pale kwa hivyo labada unakuwanga nyumbani una mswada mbali ya kuuliza swali. Lakini wacha tuanze na utaratibu wa ndio utatuzaidia na bona umefifia kwa Ben amekuwa akibeba mkono tangu katikati ya …….. (inaudible). Wacha tumpe nafasi ya kwanza. Wacha kwanza nichukue wale watu watakao …………. Baada ya Mhesimiwa Mzee, Bwana Kisia atakuwa mbili haya. Tutachukua mawali matano wewe kwanza, wewe wa tatu, tena utakuwa wa nne, mzee mwenye tai pale wa tano. Haya tuko tano kisha tuliize watu wa hapa assistant sasa tunaye. Wacha watu wako karibu na micro-phone ili muulize maswali yenu kwa urahisi. Asante.

**Mhesimiwa Samuel Kisoro**: Asante Commissioners, Githu au Muigai, Muigai sorry asante sana na wananchi watukufu wa Tom Mboya, mimi nashukuru sana, kwanza nashukuru sana kwanza nashukuru Mungu wakati mlianza hii kazi ya Commissioners wengi wetu tuliomba Mungu sana kusema labda hii Commission inatufikia njiani lakini mapenzi ya Mungu karibu mkamilize. Kweli mkasane na hii Katiba mtumalizie. Tumengoja sana kwa hamu na tunasema kwamba ikiwa Mungu anafikia na ikiwa katikati kwanza mimi hapa ni na kura. Siyo? Waamua kupiga kura popote. ……… (inaudible) kwa sababu watu wanaharibu Katiba. Sisi tunataka Katiba imalizike kisha isaidie kila mtu mlemavu, kiwete, kisiwi, mzee kama mimi au mwanamke.

Sasa swali langu ni moja. Katiba ingine nzuri………….. (inaudible) nzuri kabisa kwa sababu kuna watu wa salvation itaenda kumaliza mambo mengi. Mimi kufikia afisi hii ya Katiba sijapata sehemu ambayo hiyo Katiba inatendea mtu mnyonge. Zijapata kweli. Sababu mimi ni Bwana watoto wa kubwa na wadogo. Saa hii nitaenda kuangalia kama wana imani ndani yao. Nanunua sweets naweka kwa sahahni. Na wambia hawa watoto mtumie nguvu kila mtu apate hiyo sweet. Na wanapotokea nguvu Commissioner niko na wadogo wawili msichana na kijana wanakuja hapa ……. (inaudible) sababu wale wadogo wanagania wamemaliza.

Uzito weka Katina hii ilinde kabila ndogo na kabila kubwa. Kabila ndogo inateketea nguvu yake, itapewa kura yote inachukua vitu vyote vyeupe, inachukua councilors yote, inachukuwa Commissioners wote, tena kama tulivyofanyiwa sasa, kabila ndigo watafutwa pole pole.

Commissioners Muigai ogopa Mungu, fanya haki kwa wana-Kenya hatutaki maneno ya Katiba yetu sasa bado miaka miwili tena tunaanza kusema tunataka ku-change Katiba. Tunataka Katiba ya kusaidia mimi mwisho na watu wengine kwanza ili kwamba kila mtu afurahiye hii ya Katiba. Hatutaki Katiba ya kupendelea upande moja, upande wa ardhi, upande wa vyeo, upande wa nini tunakataka tafadhali vile kujenga tu. na mimi naomba Commissioner Yash Pal Ghai kwanza wale Commissioners, wale walikataa ku-sign hiyo Katiba hata wako na taabu sana. Commissioners hawa wapya pengine ulitumiwa na haki Kiano wanakwambia …………… (inaudible) sana. Hata wao mlikuwa kufutwa kwa kazi, kwa hivyo sababu hawaelewi raia ya watu. We are supportful those who have spoken yet …………… (inaudible) yet na vile Yash Pal Ghai si mtu wa Kenya hapana sio mhindi amefanya kazi nzuri. Pia tuendelee namna hivyo Madam na tufanye kazi kwa wageni. Kwa hiyo machache mawali yangu imemalizika ……… (inaudible) maswali tutumie tu kidogo. Asante. Majina yangu naitwa Samuel Kisoro Moibet na mzee moja hapa Kitale. Asante.

**Bwana Satia:** Asante sana. Mtu wa pili tafadhali aanza kutaja majina yako. Halafu tundelewe.

**Eliud Kisia:** Vizuri. Commission ambaye ametumwa Kitale na wale wote ambao wamefika hapa kutoa maoni jina langu naitwa Eliud Kisia, mimi ni Chairman wa KUPET Tranzoia. Nasikitika nakuja baada ya mwana siasa kuweza nikawa na challenge kubwa. Nataka niseme hivi kwamba maoni ambao tumepata katika hii draft ni maoni amabo inatoa mwelekeyo lakini sisi ambao tulikata pengine ningezitishwa kwa sababu kuna watu ambao huenda waisome Katiba ambao tumepewa na watailewa barabara.

Tutanataka sisi kama walimu na watumishi wa Serikali kwa ujumla itajwe kinaga maana wajibu kwamba sisi ni ni baadhi ya wananchi wa nchi hii. Tulipata una citizenship halafu tuko na Rais ya kumpata Defensive College kwa sababu kila mahali tumeambiwa waalimu na wafanyi kazi wa Serikali wasikilishi katika siasa na mnajua consequence ni siasa, kuzaliwa ni siasa, kutenda kazi ni siasa, na popote tuko ni kuwajiri ya kisiasa. Kwa hivyo tupewe nafasi ya kushiriki katika siasa. Ndiyo maana tunaona mambo yote inatupuliwa hapa na pigwa kama mpira hatuna msimamo, hatusikizi tunapigwa kama mpira, hatuna

msimamo, hatuzikizi hata wale walituma pale katika bunge bahati yao wamesahau kwamba walienda kama waalimu. Wamewacha waalimu wamahangaika hupo, tunakimbishwa hapo, tunatupwa hapa na pale kwa sababu ya kutetea maslahi yetu. Na hatutei kwamba tunataka tupate misahara, mbali tunatetea kwa kila ambacho tulihaidiwa.

Wale Commissioner ambao wako hapa wakitaka nyumbani wasipoenda na mahindi, kupelekea jamii yao hata wa kutoka jangani ulienda lini Kitale. Tumekula mchele tumechoka. Kwa hivyo tunaomba hivi kwamba tume ionyeshemambo wazi ni kitu gani wanalenga na iyeleweke vizuri kwa sababu tunataka tukapoingia katika uchaguzi tusaidia kama raia ya nchi watusaidie kama waalimu, watusaidia wafanyi kazi wa Serikali. Na hii mambo yetu ambao inaendelea kwa sasa inaguza kila mtu, inaguza kila mzazi au kila aliyepiga kura kwa sababu wote wana kura na wameumia tayari. Wazazi hawapendi kukaa na watoto nyumbani, embu niulize hawa wako hapa. Mumefaa watoto ugali kwani?

**Audience**: Hapana.

**Eliud Kisia:** Hawajafulani. Watoto ni kati ya waalimu, waalimu wakae na watoto na tunaweza kukaa na hao watoto mwaka mzima iwapo watapata ujira mwema. Ujira wa end month.

Tuwache ile pengine nimeseme hivi kwamba katika sehemu ile ya Parliament. Tumeambiwa kwamba Parliament itakuwa Nairobi. Lakini tume haijatuambia kama hii Parliament itakuwa life covering kwa radio na kwa TV. Kwa sababu baadhi yetu unaokuta ambao hatujawai kwasikia, na baada ya kuchaguliwa tuwaone vile kisemwa na kiongozi wetu ya kwamba tumechaguwa na wanaenda watoto wamezaliwa unafika miaka kumi na nane hawawezi kutambua mjumbe wao. Tunataka tuone wajumbe wetu kwa TV madam.

Mwisho nikimaliza nataka nisema hivi kwamba pia Commission ifikilie sijui kama itakuja namna gani kwa sababu mambo ambao yanaadikwa kwa hii Katiba mambo ambao itakubaliana agreement ambao imeingia mtu mmoja asiye na uwezo wa kuweza kutupilia mbali peke yake. Nasema hivyo kwa sababu unaenda kufungua mahakamani kwa sijui siku nane mfululizo tukingoja uamuzi wa ile mambo Waziri Henry Kosgei aliofanya kufutilia mbali lile jambo au agreement ambao tuliingia na Serikali. Kwa hivyo tunaka tume ionyeze wazi kwamba agreement ambao itakuwa imeigaziwa mtu mmoja hawezi akaitupilia mbali. Kwa hayo na mengi ambao wengine watasema ni asante.

**Bwana Sasia**: Tafadhali labda mgeni wa pili, tafadhali, kabla yule wa tatu. Tafadhali tukubaliane. Tunataka tumpatie dakika moja tu kuuliza swali halafu tuendelewe. Na pili usitaje majina ya watu kwa sababu katika tume hatujadili watu. Tunajadili firm Constitution, tafadhali.

**Com. Salome Muigai:** Tumekubalina kuwa kila mtu ana haki ya kuzungumza lakini pia nimekubaliana hakuna kazi isiyo na wajibu. Sasa leo tumepata haki zetu za kuelezea habari ya Katiba yetu na pia tumechukua jukumu letu la kuelezea na

kuzungumzia hiyo mambo tukiwa na wajibu. Na wajibu wetu ni kulinda kila Mkenya mwingine ukitaka kuzungumzia juu ya Amin naweza. Lakini ikiwa ni Mkenya mwenzako lazima ufanye nini? Umlinde ukizungumza wewe mwenyewe. Ningata kuwa kuzikiza vile Bwana Chairman amesema kuwa ukitapa nafasi una dakika moja, 60 seconds kuzungumzia ile mambo unataka ndiyo kila mtu apate nafasi. Tafadhali ukizidisha hiyo ni ile haki tumekupa lakini tumesema kila haki ina limitation ya basi ya limitation ya chorus ni ya yako, ni ya kuu, kuwa wewe mwenyewe unajili nafasi hiyo. If it takes more than one minute we are going to stop it. Thank you very much.

**Gregory Kipkemoi:** Thank you very much Commissioners, me I will speak in English. I just say ………… My names are Gregory Kipkemoi Keiyo. I can say in support of light skin in this particular Constitution vetting and we should all of us forfeit Coast Province ………….. (inaudible) a few hopeful Kenyans because I don't fear against land tribal clashes as addressed in the constitituon. My ……………. (inaudible) there is the question of land let the Constitution or value the land we are paying for public community at the private, the former white settlers should be clearly defended whose land to take, or we should say in the Constitution properly who said they took woodland ………….. Inaudible. I have said because kwa madam it is pathetic for the purpose we should know whose land is it and I think the other thing is to face it we don't know what investigation again. The government know we have been asking Njonjo Commission, we have Akiwumi Commission, we want to resolve to investigate at what …….. just the form of a second fake for those ones which were deserted. Thank you.

**Bwana Sasia**: Thank you asante sana, it is…………….. (inaudible) and clear.

**Godfrey Nyangori:** Kwa majina naitwa Godfrey Nyangori na mimi ni viongozi wa taifa wa kanisa katoleki. Na nina maswali machache. Swali la kwanza ni hapa kuhusu vijana. Na kuhusu vijana ningependa katika Katiba ……………….. (inaudible) kile ambo kimekuwa katika very appraise lakini kuna issues zina jaribu kueleza haiko best placed in the Constitution. Na inapatikana kwamba pia sisi kama vijana tuko na our host security problem ambapo hazijakuwa elewa kitambo sababu wale ambao wana picha zetu hawajui shida zetu na habari kama employment, mambo inahusu jamii kama immoralities and other issues.

Pili, swali langu linakwenda kwa sababu ya Executive. Kuna swala liliongelewa kuhusu Cabinet Ministers na because tumepewa pendekesho kwa sababu support ile tumefurahi but again ………….. (inaudible) ningependa kutoka maoni yangu kwamba the issue of Deputies Ministers because they are actually just ceremonial na already kuna Permanent Secretaries pale chini na kuna Under Secretaries. Kwa hivyo they should heed the call by refusing some of these ceremonial positions.

Swali lingine ni kuhusu shamba, hasa kama mkaazi wa hapa Kangoya kuna mashamba ambao ndiyo tunasema kwamba kila mtu apatiwe shamba. Lakini hasa kama hatukawa I think it is a very essential place whereby around 7% of squatters reside such as the country club. Tumepewa medhali fulani kwa wale watu ambao wana mashamba na hawasili kikamilifu. Kwa sababu hilo ni swala ambao zinafanya production sijui inarudi chini. Mtu ana shamba twenty five acres and above na is not utilizing them.

May be haya ndiyo maswali yangu matatu . Asante.

**Kennedy Guya:** Kwa majina naitwa Kennedy Muya mimi nafanya biashara hapa town. Na nina maswali machache ya kuuliza. Nikaona kwamba katika Katiba hii ambayo inaindikwa pia kuna devolution government. Na ukizali kidogo unaleta ni kama sasa hata kama haijakuwako ime-make Local Municipal Councils an Town Councils kuwa expert but ukiona ……….. (inaudible) sasa sijui kama tuta prevail Municipal Councils to handle Town Council that is my first question.

Basic Education: Kuhusu Education wamesema kwamba kutakuwa basic education. hapa Basic Education katika watu ni Primary peke yake ama ni Secondary Education. Na kama nitamaniza Primary peke yake Katiba imekuwa worthy leo tutafanya kutengeneza Primary Education na Secondary Education kwa heavily Kenyan citizen.

My third question goes to the labour. Nataka kuzungumzia juu mishahara na deni. Kama unajuwa kwamba watu wengi wanategemea kazi. Na the guest of honour wanaweza kumalisha ………… (inaudible) wanasoma lakini hawa ku-product kwa hii kazi. Katiba itafanya ………… (inaudible) hata kama umendelea Bible you pass uwe nafasi number one utafanya je kazi katika hizi uweze kuwa productive katika kazi.

My last question itaenda kwa President. tumezungumzia kwamba President akuwe between 35 and 70. Suppose sisi tulikuwa ……… (inaudible) candidate towards 69 years, my first child atafikiza seven, do I have to fight between there ama ile itafika wapi?

My last question iko kwa MP. Tumesema kwamba tuna right ya kuita MP wetu nyumbani. …………. (inaudible) wambunge hawapatikani kwa urahisi. Je kama tunamwita kwa gazeti wananchi watafanya nini?

**Bwana Satia**: Asante sana.

**Tom Were**: Hii Commissioner na wote tumefika asante. Majina naitwa Tom Were na nilikuwa ni mfanyi kazi lakini nitaomba niongee kwa kizungu.

One thing that I am really having a problem is about land and especially what you call Public Lands. What I have had is this, there is this public lands that we have at ADC farm, KARI farm that have already changed hands that four/five times. The original people who grab the land are not in the books, but what is the Constitution is going to do about it. How are we going to address the issue who bought innocent;y for grabbers and the Constitution say that they are going to possess Private Lands. Somebody bought land from somebody who grabbed it and it is five half down the road and we want to address that issue per further because like in Kitale, Kitale basically is an agriculture area. We cannot operate without ……….. (inaudible). Anybody anywhere you go round you find others in grabb. So the first thing we have is very clear in the Constitution. We are going to protect private lands that have already been acquired locally. We are not going to protect lands that tranverse fraudently so. That is my first question.

My second question go to if anybody going through the Constitution they got what we call what other the Bill of the Rights na the ………….. (inaudible) mean that if you are going to an election it is going to be one month old. But looking at what the provincial had Draft Constitution there is a section of the number where they are putting some bills for special interests. Now how are we going to address the issue ardth, I am finding people are wrestling in my area and then I look for…………… somebody else comes in ………………. (inaudible) taking part they have a special difficult put for them. So are we going to put the details that we need to be addressed.

My third issue in law there is only customary law when you look at chapter for the Draft Constitution the law that applies in Kenya Constitution enacted law and then Customarily Laws. There is no many people ………………… (inaudible) who want to know Customarily Law basically is personally law and when we come to personal law how is the Constitution to protect our rights it is due with inheritance, marriages, and everything but in the first part the Bill of Rights you can address issues of about crimitation of jobs personal law. So those are my questions but what ……………… (inaudible) the support the land issues because unless we address this problem, down the road we have to send the same same problem is it a first class and somebody be happy to have no land. It has to come back to the public, belong to the public. Thank you.

**Bwana Satia**: Anza kwa jina lako halafu mawali.

**Patrick Birech**: Kwa majina naitwa Patrick Birech mkaaji wa Tranzoia. Nina maswali matatu. Ufisadi: Swali la kwanza napenda kuuliza kuhusu mawaziri na wabunge hawa. Umezungumzia kuhusu waziri, kile ambavyo wanakudhuru kwamba siku ya leo ni vizuri nipati na nikauliza swali. Je kwangu ameteliwa mbunge tuliochagua atuwakilishe achaguliwe kuwa waziri halafu baadaye hatimaye afutwe kazi, ama na akiziuzulu hapa tumejuwa ya kwamba tutachagua mbunge mwingine wa kutwajiliza tena. Je yule akifutwa kazi ataenda wapi? Swali limeweleka? Akifutwa kazi ya uwaziri ataenda wapi? Na si tulichagua hawa waizaidizi.

**Bwana Satia**: Tafadhali tunajua unanichagua lakini haya maswali yanaulizwa Commissioners tafadhali. Kwa hivyo mpeni Commissioner nafasi azikize ili aweze pia kuyajibu.

**Patrick Birech**: Swali la pili ndugu yangu kuhusu mkilima, hapa Tranzoia sisi ni wakulima wa mahindi na vilivyo twa twatoa maziwa kwa wingi. Watu kama tume toa mazao yetu kama hizi, tunaweza kupendekeza bei tunaotaka ama mtu mwingine ataingilia card? Kwa mfano naweza kusema ………….. (inaudible) mwaka huu tunauza mahindi kwa shilingi elfu moja mia nne. Kuna mwingine atapinga? Halafu vile vya maziwa tutaenda kutoka maziwa halafu tunaweza kuona kuwa maziwa ambao tunatoa kwingi ama tunasema ya kwamba maziwa yetu tunauza wapi na bei tunauza namna gani. Vile wakulima wengine na wafanyi biashara kati kuingilia. Hizo tunaweza kuweka bei yetu sisi wenyewe ndiyo ni swali la pili.

Swali la tatu ambayo ni ya muhimu inahusu …………… (inaudible) uhuru wa kuabudu ile nataka nijue leo ni kweli. Mimi mwenye nilikuwa mshiriki wa Seventh Day Adventist Church. Tunamnavyojua kuwa sisi wenyeji tuna uhuru wa kuabudu kuwa siku yenyewe ambayo inahusu tuseme consult na watu wengine ambao wangetakikana waende kazinisani lakini wazee wengi wasiejaa hata wa Yesu siku hiyo kuenda kanisani, hawaendi, akiwachwa ni lazima ufanye kazi siku hiyo yenyewe. Je, hatuna sisi wote tulio jumapili na Mislaam yule ambaye tena ……….. (inaudible) siku ya Sabato je una uhuru wapi wa kuwabudu. Asante sana tafadhali sijui itakuwaje tuseme mambo yetu yalingana na ………………..(inaudible).

**Bwana Satia**: Asante sana.

**Ismail Masika Masinde**: Kwa majina ni Ismael Masika Masinde. Swali la kwanza ningependa kuuliza Commissioner kwamba katika redeem of Jeshi ya Housing, nyumba na chakula. Naelea kwamba watu wa Kenya kukuwa na tabasamu ni lazima uwe na mahali pa kulijenga. Wale chakula sasa vizuri unde milima na watu wengi wa Kenya ama wa chache hawaishi katika mashamba yao. Wanaishi mahali ya kukodeza wananchi lingine labda kwa mabavu je mimi naongea sijakuwa na nyumba safi na tangu nikuje hiyo kwa hiyo nyumba ama ……….. (inaudible) lakini hamjaongea vile ambao hawana mashamba wataishi mahali gani. Watapa wapi mashamba?

Pili, watawesaje kula vizuri ili watu wao wenyewe hawana pahali pa kulima?

Tume bado haijazungumzia vile watu ambao walitolewa katikamashamba yao katika clashes ya 1992 na 1997 kama watarudishiwa mashamba kama yatafanywa hivyo sababu haitakujia hiyo?

Kama mwalimu ningependa kuuliza hivi. Pia bursary sheria inasema kwamba mzazi amechukuwa mtoto ampeleke secondary school alipe term ya kwanza, ndiyo principla wa shule angalia kama hiyo mtoto atafaa kupewa bursary.

Ikiwa wewe ni mzazi hana budi ya kulipa mhula wa kwanza, term ya kwanza, atawezeza je shule Head Master anagaliye ajuwe kwamba ni maskini ampatiye mzee bursary.

Mimi kama mwalimu nigependa ni kijiunge na siasa lakini sheria iansema kuwa sio uwajiri ndiyo watu kupiga siasa nauliza hiyo …. Nauliza hivi kwanai mwezi mzima uziwe tu mwezi mmoja nitapiga siasa na ningeshidwa darazani?

Nne, kuna vijana wengi ambao labda ikiwa wafika university hawajaajiliwa kazi. Ukienda nchi nyingi watu kama hao wameajiliwa na Serikali, wanakula mshahara kidogo, kwani ni mshahara ambao unatuma je shule, huko nyumbani wameo, hawaajiriwa, hawana mashamba Serikali ama tume kupendekeza ni jambo gani la kusaidia hawa vijana. Wataishi …………. (inaudible) wananchi ndiyo wana vyao, wataishi juu ya wazazi yao, wataishi juu ya viunda, wanaishi mahali gani? je tumeshafikilie hao? Asante sana.

**Bwana Satia**: Asante sana.naona kwamba amesema kweli zaidi. Labda sasa tumpatie Commissioners nafasi ajibu haya maswali kwa sababu ya katikati halafu tutafuata pale. Kwa hivyo Commissioner karibu.

**Com. Salome Muigai:** Asante sana Bwana mwenyekiti na asante wenye kuuliza mawali haya ni maswali mazuri, pengine unamzikiza mtu nafikilia hili awali niliasikia Mombasa ya kuweko kwa hayo maneno exact words sisi wenyewe tulikuwa tunatatishwa na hayo mambo mengi yenye mumeleta leo. Lakini sasa namuona haya Bwana Moi Ben amenda kabla ya kujibiwa swali fulani kwa hivyo pengine tutaliacha, tuwaze na Bwana Kisia, andikiza njia ya kuwasaidia watu wanyonge na tukasema ndiyo kwa ajili tunaleta Serikali karibu na watu ili tukifikilia watu gani wetu tunafikilia unyonge na nguvu za watu wetu. Kukiwa mtu mwenye anafikilia hiyo habari ukiwa Nairobi kuna watu wengi wenye hutakumbuka. Lakini ukiwa unafikilia watu kuwa Kitale utakumbuka watu wako. Tumesema watu kama walemavu lazima wahuzizwe kwenye decision making mechanism, lazima kuwe watu wenye kushikilia haja za watoto, lazima kuwe minority katika uhuzizaji wa the Local Government, the guards at the locational level lazima ihushishwe kila mtu mwenye uko hapo ili matakwa ya kila mtu yakwe. That is very clear in the Constitution.

Lakini pia zakubali kuwa hii Constitution husomi mara ya kwanza na kufuata kila jambo. Wakati mwingine ukitoa mara ya pili na ya tatu ndiyo unasema oh kumbe ndiyo this part ina je-suit my idle shoes. Kwa hivyo ndiyo tunasema pia kama tukiwezeshwa kuwa na election tofauti kama hizi zenye tuko nayo sasa zimekujwa mix proportional representative hiyo pia litawazeza maginals strike watu wenye numbari kidogo sama huweza pia kuhuzishwa kwenye ubunge. Meshimiwa akuwa hapo wakati nilizungumzia juu hayo kwa hivyo wengine wale tulikuwa nafikiri tulikuwa tumesema.

Bwana Kisia na habari ya waalimu na wafanyi kazi wa umma na siasa pia iwe imerudiwa na mzungumzaji wa mwisho. Katiba ya wakati huu imewakubaliza Waalimu na wafanyi kazi wa Serikali kuchukuwa leave kuwezeza kutuhutiza na habari ya siasa. Lakini pia ni haki yenye pia ina wajibu wake na juku yake. Je mimi nikiwa ni mwaalimu, ni headmaster wa shule fulani, shule gani iliyo karibu hapa? Kitale Academy ni shule ya kibinafsi au ya Serikali?

**Audience**: Ya Serikali.

**Com. Salome Muigai**: Ya Serikali. Kitale Academy? Na mimi ndiyo Headmaster, mimi nimeenda nimefanya nimepiga siasa mtu mtaa ende apige siasa nimekosa kupita rafiki yangu hapa amepita, watoto wake watatu wako shuleni mwangu. Na husiza sisi watoto hao kwenye shule mimi ni na baba yake ama mimi na mama yake tumelikuwa tunangania kiti kimoja. Kwa hii ni wakati wa Wakenya sio kukiuza Katiba yetu peke yake lakini kujigeuza nia sisi kwenyewe. Kujua kuwa nikipatiwa uhuru una jukumu.

fulani

Parliament – Life covering: Pia Parliament itakuwa ikinukuliwa moja kwa moja na vyombo vya habari kutujuliza sisi. Iko kwa Katiba.

Pia a recent swali juu ya mamlaka nyingi kuwa kwa mtu mmoja hiyo pia tukizungumzia ulisikia vile lazima mtu mwenye kutumiza mamlaka fulani azungumzie na awasiliane na watu wengine. There is a lot of negotiations and a lot of consultations before anyone person can make the final decisions. So it is not the time when you are making a decision in a insolation, is a time of a lot of dialogue and a lot of listening to people who will have to make the decisions.

Gregory alauliza kuwa tusiwache watu wawili hapa watatu wahalimbu hii Katiba hii ni kati ya wananchi zina la kujibu la zianda lakini nataka pia tuweleze kuwa white highlands ilikuwa zalani. Mimi sitaki kusema, Katiba haijasema white highlands zilikuwa … lakini pia ningetaka kuwambia vile nilivyosikia nilipokua nikichua maoni ya watu. Nilipoenda Marakwet, Wamarakwet waliniambia wana jukumu kubwa sana, wana kazi kubwa sana ya kuzaana ili watu wachukue mashamba yao. Na haya mashamba iko katika Marakwet, iko Uasin Gishu, iko na Tranzoia. Nilipoenda Elgon, Wasabaot waliniambia wako very busy wakifanya nini? Wakizaa ili watu wasichukue land yao yenye Elgon na Tranzoia na wapi? Na Bungoma.

**Audience:** Bungoma.

**Com. Salome Muigai**: Na Bungoma. Nilipoenda Kajiado niliambiwa Wamaasai wako na kazi kubwa ya kufanya nini?

**Audience:** Ya kuzaana.

**Com. Salome Muigai**: Ya kuzaana ili watu wasichukue mashamba yao. Na mashamba yao ilitoka Uasin Gishu, Nakuru, part of Tranzoia. Sasa hiyo inajieleza kuwa Wana-Kenya inawezekana turudi tufikilie land ilikuwa ya nani. Moja wa watu tume Tobiko aliniambia unaona KICC iko hiyo ilikuwa machacha ya babu yangu. Unasikia? Naye mama yangu ananiambia unaona pahali panaitwa nini? Pahali St. Mary's mtoto wangu anasoma St. Mary's. hiyo ilukuwa shamba ya babu yangu. Sasa sijui kama mnataka tuanze hapa twende mbele ama tutachukuwa nafanyi ya kurudia chakalme vipi zenye ziliicha, sisi wenye Kenya itatubidi kufanya very very hard decisions ya kufikilia tuko wapi wakati huu hiyo ndiyo yenye tumeangalia. Sivyo? Pahali gani tuko. Tunaweza kufikilia sasa vile tuko hapa pengine tumefika Nakuru, tutarudi Tranzoia ama tutaenda tena twende Nairobi. Na hiyo ni decisions siyo ya Tume ya Katiba, hiyo ni decision ya nani? Ya wana Kenya. Kwa hivyo mkija sisi wakati wa National Constituency mutwambia turudi nyuma, tutarudi. Mkitwambia twende mbele, tutafanya nini? Tutaenda mbele. Sisi tunatumikia wananchi wa Kenya.

Kuna swali lingine lenya liulishwa juu ya Basic Education. Basic Education ni kutoka Pri-Primary mpaka Secondary school. Kwa hivyo hiyo itandikwa hata ile maswali ya shida ya bursary ndiyo yenye tungetaka kama ingewezekana iwe ya bure.

Pia ningetaka kusema ukiwa ukipatiwa haki, sio kusema lazima kesho Serikali ifanyishwe hizo haki zote. Haki za watu ama Katiba ya watu pia ni mwelekeyo wao. Kuna mambo ingine tunaweza kufanya leo, kuna mambo mengine tunaweza kufanya baada ya miezi tano ama sita, kuna mambo mengine yenye tulikua miaka tano kutimiza, kuna mambo mengine yenye tutakua bado tunajaribu hata wakati Yesu ataporundi. Si ndiyo? Kwa hivyo lazima tuelewe kuwa Katiba ni mwelekeyo ya, is road mark, ni kama kusema ina road mark ya kutoka hapa mpaka Nairobi. Ama tuna road mark ya kutoka hapa mpaka Kampala. Hiyo siyo kusema lazima baada ya dakika tano tufike, inawezekana? Basi tuchukue nafsi yetu lakini tutakua tukipita pahali tunaweka nini? Tick. Tukikaa muda mrefu pahali moja tunaweza Nairobi bado tuko Masinga bado ya saa moja, sisi tutaanza kupiga kelele? Tuseme, tuseme tunaenda Nairobi, tulikuja tukafika Masinga, tulikaa hapo Masinga sana. Lazima tufikilie kuna shida tatu usiku. Kwa hivyo Katiba yetu mambo mengi ilioko inaweza kutimizwa lakini mambo mengine yenye ina road mark na ina wakati wake wakufanyika, na ingine intachukua muda mrefu kuliko mwingine.

Ninaulizwa swali juu ya employment, kuwa kama Katiba inasema nini juu ya employment, kwanza tumesema kila mtu apate kazi ngapi? Moja. Hiyo infungua nafasi kwa watu wengine kupata nini? Kupata kazi. Lakini pia tumesema watu wa Tranzoia wakikutana wafikilie kitu chao kikubwa ni fahari yenye wanapata factory zenye zitatumia, kufanya mahindi kuwa chakula, kuwa cereal, kuwa unga ya mahindi, kuwa chakula cha kipi tutafanya mgogoro kuwa fertilizer, hizo factories ikianzishwa hapa kwani itakuwa priority zenu. Itapeana nini?

**Audience**: Kazi.

**Com. Salome Muigai**: Itapeana nafasi ya kazi? Kwa hivyo hii habari ya kugeuza Serikali inje karibu na watu pia hiyo kwa upande mwingine ni mbinu za kuanzisha kazi pahali tofauti. Watu wa Kisumu wakifikilia wanataka fulani wa kutengeneza samaki kule basi itakua pia nini? Ni nafasi ya kuleta kazi.

Na pia kwenye hii Katiba kuna mambo mengi yenye imeguziwa, imefukuza, kwa hivyo ni nafasi ya kila mtu kuisoma yenyewe every article and relating some article to others to be able to understand which issues are being taken on board and then if you find that there is one or critical issues that have not been taken on board, please make proposals.

Again si kutuliza mawali tuelezeni kama tungefanya hivi pengine tungezaidika hivi. Ukitupa hizo proposals tutazirudisha tutaziangalia tena na tuta zenye zinawezekana tunapeleka kwenye Katiba. Kwa hivyo tafadhali usikue mtu wa kusema unaona vile mtu kama amesimama kado ya football unaona vile amefanya hiyo mpira. Eleza kama huyu mpira alivyoufanyia hivi tunge shinda. Basi zote tuko kwenye hii barabara.

Presidential age – tumesema kuwa itakuwa miaka sabini. Mtu wa miaka 69 hajafikiza miaka sabini. Kwa hivyo ataingia. Mwisho wa kumaliza itakuwa miaka sabini na nne it is okay ya – tumesema tu asiwe zaidi ya miaka sabini wakati wa kufanya

wa kuingia . Akiwa ana miaka sitini na tisa na miezi kumi na moja na siku tano wakati wa election, amekubalisha. That is the law. Hajafikiza miaka sabini.

Lakini pia niliweleza kuwa kuna trantional mechanisms. Kuna mipatilio yenye tumeleta ili tuweze kutoka kwa mambo ya kale tukienda kwa nini kwa yenye tunaenda mapya. Kwa hivyo ule uchaguzi wenye utafanywa wa kwanza wa Katiba mpya, unawezekana ukiwa afanyiwe akiwa na miaka sabini.

Kwa mengine watu tayari walikuwa kwenye hiyo process. Hutaki kufungia yule mmoja mpaka ukaonekana kumbe imefanya nini? Imenunuliwa na fulani ndiyo inaweka hiki kiwango ndiyo kufungia inje. Kwa hivyo in transitional period tunaipa nafasi ya kutoka kwa one place to go to the other place without too many casualties. Kwa hivyo wakati Wakisii ni wa kutoka wapi? Ni Wakenya wana haki zao, wamelindwa pia. Hiyo habari yakuwa tunaweza kumwita tumwambie MP atoke bunge akataye, hiyo habari tumesema kuwa tunataka we want to become a country that will be lead by rule of law. Ikiwa sheria zasema hivi too bad. That is the law. Hiyo ndiyo sheria ondoka. Hatutaki habari ya sheria ina apply differently. Tukisema tunai-quote before the law we mean ile sheria itaniangalia ndiyo vile itakufanya nini? Itakuwangalia.

**ADC AND KARI LAND**

I would like you to make proposals. Tumesema kuwa mleage lands italindwa lakini pia tumesema from no as it was acquired legally. Kwa hivyo una nafasi ya kurudia hayo mambo yenye imefanyika mbeleni. Lakini pia tungetaka proposals kama ina proposals yenye zinaweza kusaidia. To be alert protecting lands that was illegally acquired. Tumesikia kuwa such lands have been grabbed. Give us proposals how to deal with that.

Umezungumzia habari ya equality versus affirmative action. Kwa nini tunasema mtu mmoja aende atokwe na jasho kabisa akipagania kiti na mwingine apewe tu. We are accepting injustice of the past. Tukisema kuwa kwa mwaka ambapo imepita mtu mwingine alipaguliwa. Lakini tukisema kutoka leo hapaguliwi lakini aanze tu pahali alipo. Akaanza mwenye alikuwa mbele for example kama mimi nimekuwa nifanyiwa – tunazungumshia habari ya mtu. Mimi nina ulemavu ya kutembea, sasa twajua wewe tumetoka hapa tumetendea masaa ishirini. Mimi niko sijui wapi nimefika hapa kwa Akanyeni, wewe umefikia wapi after 20 hours. Si utakuwa umefika Eldoret. Sasa kutoka leo mtembee kila mtu anaweza kutembea kwa the same pace.

Kuna wakati mtamsikia. Si lazima mtu mmoja aseme lakini yule apewe tu tafuteni for supporter. Ni mkimbizi afikie nani? Ingawa afikie yule ndiyo waweza kutembea pamoja. Kwa hivyo tunasema pahali penye pamekuwa ubaguzi lazima tufanye jambo fulani ili tuwezeshe kuwa na tukiwacha za kuchezea zenye nini? Chenye usawa. We have to do some affirmative action so that the reason why we said such people should be given a chance to catch up a little bit with the others.

Pia habari also equality. Tukikubaliana kuna equality pengine inatubidisha kusema equality is not sameness. Kusema tuna hako sawa siyo kusema tunatosana ama tuko sawa. Kwa haya zaidi have been Kiswahili. Equality does not mean same for example

tukisema mtu mwenye ulemavu is equal to the one without ulemavu tumesema umefanana.

**Audience**: La.

**Com. Salome Muigai**: La, tukisema Mbukusu na Mkikuyu ni equal tunasema wamefanana?

**Audience**: La.

**Com. Salome Muigai**: Mmoja kuona kama anasema hakuna chakula, mwingine akipata hakuna githeri ansema hakulicha. Tukisema they are equal in kusema huyo wa footman tupatie optsman akuwe amekula chakula. Yule wa team tumpatie …….. (inaudible) Mwenye anataka githeri, tumpatie githeri. That is equality. They need to be treated equally not necessary the same. Tumelewana hiyo? Tukisema watu wote ni equal basi watupatie githeri wote it won't work.

Equality pia ni kusema mtoto ulemavu na mwenye hana ulemavu they are equal. Sasa ndiyo tutafikilia huyo mwenye hana ulemavu,hata kimbia aende shule yenye iko karibu. Ndiyo wakati huyo itafikilia pengine we need more – what are they called? More places where the disabled children stay. Hapo kwa shule, tunasema watoto wengine waende nyumbani wale watakimbia wafike shule kesho lakini tutengeneze pahali fulani yenye mtoto mlemavu anaweza kulala karibu ndiyo aweze kufanya nini. Kusoma. Ni kwa vile tunasema they are equal. Lakini hao kutekeleza hiyo equality ni lazima to order another third point equity. If chooses a way of showing equality. Tunelewana? Ndiyo tutapewa mtoto mlemavu anahitaji either apate bus ama apate boda boda he has to be helped ndiyo aweze kufanya ile kitu mtoto yule mwingine mwenye hana ulemavu anaweza kufanya.

So lets understand the principles of equality does not mean them. When we say them as women are equal we don't mean they are the same. Kila mtu anajukumu, ana kazi yake. Lakini tuwekee manani hizo kazi zote. That is all we are saying.

Then we have talked about Customarily law versus the Constitution. Constitution imekataza kubaguliwa. Nobody should be disciminated against either on graze, religion, ……… (inaudible) disability ama chochote kile. So tunakubali Customarily Law so long is it does not discriminate. Discrimination is a negative principle, tumeikataa kwa hivyo every law customary law utamaduni wetu utakubalika kwenye Katiba ikiwa ulevi vitu vienye tumezafanya nini? Tumezakataa. Tumelewa hiyo. Therefore every customarily law that discriminate it is cut. And let me give you an example. Zamani ilikuwa ikiwa Mkikuyu lazima uende uimbe ulete ngombe za Wamasaai ndiyo ukileta kushindi ya kiasi baba yako atakuongeza kiasi fulani ufanye nini? Uoewe. Sasa bado utakasoma ni hiyo uvivu. Sasa tukiweka leo kwani utamaduni wetu ni mzuri, tutakuwa na amani wakati wa Wamaasai na Wakikuyu. Na tunataka kukaa na amani. Tunataka kukaa na amani. Kitu kikubwa kukaa na amani na kabila zingine ama utamaduni wetu exactly live will make choices siku kwa siku.

Maisha ni habari ya kufanya nini? Ya kuchagua. Kitu kikubwa kuliko chengine. Wakati mzazi anafikilia kulipa 40,000/= kwa university mtoto aende university, ni kwani hiyo pesa haikupata kazi ingine ya kufanya? Ni kwani kulikuwa hakuna kazi ingine. La hata saa ingine amefikilia tuweke mabati kwa nyumba yenye bado ina nyasi. Ndiyo huyo mtoto afanye nini asome. Kwa hivyo maisha ni uchaguzi. Making of choices, so even in our Katiba we have to keep on making tracing.

Patrick ameuliza habari ya MP mwenye amechaguliwa kua waziri kwa hivyo itambindi kufanya nini? Kuacha kazi ya kuwa MP mbunge aende akafanye uwaziri, je akikutwa kwa huo uwaziri bado ni nini? Na tulisema nini mwishoye, tunasema life is about choices na ni haki ya kusema mimi sitaki kuwa waziri nitaweka kiti changu cha mbunge after all I have for five years. Lakini pia Katiba hiyo yenyewe imesema hata hii tukisikia kiti ya mbunge, tukufanya ukaguzi wa kuona kile anafanya nini? Anafinganya anapoifanya kiti cha kufanya nini?

Ameuliza kama wakaji wa Tranzoia wanaweza kufikilia bei yao. Dunia ni soko Bwana Patrick. Kuna mzaji na kuna nini?

**Audience**: Mununuzi.

**Com. Salome Muigai**: Kuna mununuzi. Ukikata bei yako useme ile gunia ni shilingi elfu mbili na kupatikane mununuzi fanya nini? Uza. Lakini ukiita hiyo na watu wakataye kinunua wanafanya nini? Basi vile tungetaka kufanya ni kufanya mipango yenye itafanya soko huru la kuuzia watu vitu vyao. Lakini kuziwe kuwa mkulima harundishiwi faida yeyote. Kwani hakuna nchi ikifanya kazi pia faida haiwezi kuweka raslimani sivyo? You cannot if until you make a profit you cannot invest, and as a country we need to invest and investers alikuwa ni nini?

So this Katiba should look for ways and I would like Patrick suggestions and proposals on how we make the mkulima make a profit ya at the Market place and ensure that he has some electrol vat to be able to invest.

Pia ni hii habari ya kuabudu na dhiki ya Sabato. Huyu mjadara uliendelea muda mrefu sana lakini tukaona kuwa vile tumesema Kenya sio nchi yenye chini ya Taifa. Kuna dini nyingi na kila dini itapewa mamlaka sawa na ile nyingine. Tungetaka kutoweka siku fulani kwa dini fulani pahali fulani. Hata kwenye Katiba hatujasema siku ya jumapili ni siku ya kwabudu kwa Wakristo. Hatujasema kuwa Ijumaa ni siku ya kwabudu kwa dugu zetu Waislaam. Hatujasema siku ya Jumamosi ni siku ya Sabato for dugu zetu Seventh Day Adventist. Vile tumefanya ni kutoa utaratibu wa jumla kuwa kila mtu ana haki ya kuabudu. Mara nyingi sisi wenyewe tulipokuwa Mombasa tulijikuta tukifanya kazi Jumamosi, tulijikuta tukifanya kazi Jumapili, tulijikuta tukifanya Ijumaa saa nane ama saa saba wakati wa maombi. Kwa hivyo tukamuona hatuwezi kuidhinia ili iwe iko kwa Katiba lakini kwa ajili ya uhuru huo wa kuabudu kila mtu anaweza kuliza siku yake ya kuabudu.

Bwana Masika Masinde ameuliza juu ya chakula na nyumba ya kuishi bila kua na shamba. Tafadhali ningetaka msome vile tumesema habari ya mashamba. Na ukiona kuna jambo lenye bado haijakuwa covered properly, tupe pendekezo. Give us

proposals. Caustic proposals where we think we can be able to deal with the ………

So the land clashes na mashamba ya watu hao tumeweka human rights, tume ya human rights itangalia mambo itafanyika kutokea leo lakini pia itangalia mambo yenye imefanyika hapo zamani. Unajua Katiba ni kama Ten Commandments. Ni mwelekeyo tu. Haiwezi kuchikilia kila jambo lakini pia tumehitaji bunge kutunga sheria zenye zitaweza kutekeleza huo mwongozo wa Katiba. Kwa hivyo wakati bunge itakuwa ikifikilia, ikitunga sheria ya kuangalia huu mwongozo wa tume haki za kumlizada tutaingalia pia vile tutahuzisha ile watu wenye wamekuwa na land clashes.

Nafikiri nimzungumzia mambo yote isipokua ujana – the youth and their problems. Tulizungumzia kisasa habari ya vijana sana sana tukasema hii inatakiwa kuwa kwa Katiba kama vile wanawake na watoto na walemavu. Watu wengi walionelea kuwa ingawa ni kweli kabisa kuwa ujana una shida zake za kipekee, hasa ni mpitio tu. Wakati wa ujana ni wakati mfupi kuliko wa utoto. Mtu u mtoto miaka kumi na nane, miaka ishirini na tisa kama bado uko university. Lakini wakati wa kuwa kijana kama huu wakati wenyewe mnatafutia kazi, tunakutafutia kuwa represented ni kwa wakati mfupi. Tumesema kuwa mtu anaweza kuwa kwenda pale akiwa na twenty one years. Tulifupisha kwa ajili ya vijana. How is the habit done on that. Kwa hii mambo ya the night shift it meets proposational representation. Tumeweka kua watu wenye kuingia kwa mfumo huyo wawe pia wana ……….

Kwa meeting representation 50% ya wale watu wenyewe wataingia hao wawe ni few. Watu wanauliza watapata ni youth na wengine ni akina mama. You can be a woman and a youth. You can be disabled and a youth. You can be a professional and be a youth. So we are looking on a way for the youth to be for. Now I am going to take another ten questions.

